# BENKI YA BIASHARA MKOMBOZI

# MKUTANO MKUU WA KUMI NA NNE WA WANAHISA

29 JULAI, 2023

# YALIYOMO

1. Dira na Dhima ........ 3
2. Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Mwaka ........ 4
3. Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi ........ 6
4. Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji ........ 11
5. Dondoo za Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kumi na Tatu ........ 17
6. Yatokanayo na Dondoo za Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kumi na Tatu ........ 35
7. Taarifa ya Wakurugenzi ........ 36
8. Taarifa ya Mkaguzi wa Nje wa Hesabu na Taarifa za Fedha ........ 53
9. Pendekezo la kuhamia Sehemu ya Soko Kuu la Uwekezaji ........ 98
10. Bodi ya Wakurugenzi ........ 99
11. Menejimenti ........ 100

# DIRA NA DHIMA

## DIRA

Kuwa benki inayoongoza katika kushughulikia mahitaji ya ukuaji wa biashara ndogo na za kati kwa kutoa huduma za kibenki zenye viwango vya hali ya juu na kwa uadilifu kwa wateja wote kuanzia wadogo kabisa na kampuni za biashara.

## DHIMA

Kuwa benki itakayotoa huduma za kifedha za viwango vya juu kwa sekta zote na viwango vyote vya uchumi kwa namna ambayo ni endelevu huku ikiwajibika kwa jamii ili kukidhi matarajio ya wadau.

# TAARIFA KWA WANAHISA WA BENKI YA BIASHARA MKOMBOZI

**Taarifa inatolewa kuwa**; Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa wa Benki ya Biashara Mkombozi utafanyika kuanzia saa tatu asubuhi ya tarehe 29, Julai 2023 katika Ukumbi wa Mtana, Ghorofa ya Kwanza, Jengo la Millennium Towers 2, linalopatikana Makumbusho, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam.

## AJENDA

1. Kufungua Mkutano.
2. Kupitishwa kwa Ajenda ya Mkutano.
3. Kuthibitisha dondoo za Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 13 uliofanyika Julai 30, 2022.
4. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 13 uliofanyika Julai 30, 2022.
5. Kupokea, kujadili na kuidhinisha Taarifa ya Wakurugenzi ya mwaka ulioishia Desemba 31, 2022.
6. Kupokea, kujadili na kuidhinisha Taarifa za Fedha za Benki kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2022 pamoja na kupitisha taarifa ya Mkaguzi wa Nje ya Taarifa za Fedha za Benki kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2022.
7. Uteuzi wa wakaguzi wa Benki.
8. Kupokea, kujadili na kuidhinisha pendekezo la kuhamia Sehemu ya Soko Kuu la Uwekezaji katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.
9. Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka ujao.
10. Mengineyo.
11. Kufunga Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 14 wa Wanahisa.

## ZINGATIA

1. Mjumbe anayetaka kuhudhuria Mkutano Mkuu wa mwaka anapaswa kuja na nakala ya stakabadhi ya Hisa za Benki alizonunua au Cheti cha Hisa alizonunua.

2. Mjumbe mwenye haki ya kupiga kura katika Mkutano Mkuu atatakiwa ateue mwakilishi ambaye ndiye atakayepiga kura kwa


niaba yake kwa mujibu wa Kanuni za Kampuni. Fomu ya mwakilishi aliyeteuliwa inapaswa kufikishwa katika ofisi iliyosajiliwa ya Benki siku tatu kabla ya Mkutano Mkuu. Fomu hii inapaswa iwe katika muundo ufuatao

"**Benki ya Biashara Mkombozi**"
Mimi/Sisi.................................................................wa......................................................................nikiwa/tukiwa mjumbe/wajumbe wa kampuni iliyotajwa hapo juu, nimemteua/tumemteua ...................................................... wa ...............................kuwa mwakilishi atakayepiga kura kwa niaba yangu/yetu katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa wa Benki utakaofanyika Julai 29, 2023 na wakati wa kuahirishwa kwake.
Imesainiwa siku ya ................. mwaka .................... 2023

3. Wanahisa wote na/au wawakilishi wao watapaswa kusajiliwa kabla ya kuingia ndani ya ukumbi wa mkutano kwa tarehe ya mkutano.

4. Vitabu vyote vilivyo na ripoti za kifedha na taarifa nyingine muhimu za benki vitapatikana kwenye matawi yote ya benki wiki moja kabla ya kufanyika kwa Mkutano Mkuu.

Kwa taarifa zaidi, wasiliana na Ofisi ya Benki kwa anuani ifuatayo:
Benki ya Biashara Mkombozi,
Kiwanja Namba 40, Nyuma ya Kanisa la Mtakatifu Yosefu,
Mtaa wa Mansfield,
SLP 38448, DAR ES SALAAM.
SIMU: +255 22 2137806/7,
SIMU bila malipo. 0800 750 040
BARUA PEPE: info@mkombozibank.co.tz / shareholders@mkombozibank.co.tz
Web: www.mkombozibank.co.tz



**PAULINA KUNJUMU**
**KATIBU WA KAMPUNI**
**KWA AMRI YA BODI YA WAKURUGENZI**
**MEI, 2023**

# TAARIFA YA MWENYEKITI WA BODI

**Wapendwa Wanahisa,**

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, ninatumia fursa hii kuwakaribisheni nyote katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kumi na Nne wa wanahisa wa Benki ya Biashara ya Mkombozi. Ninajisikia fahari sana kupewa nafasi ya kuhudumu katika nafasi hii ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Biashara Mkombozi kwa muda wa mwaka mmoja na nusu hadi sasa. Ninaona fahari kuwasilisha kwenu mambo muhimu ya Ripoti ya Mwaka na Taarifa za Fedha za Benki kwa mwaka ulioishia Desemba, 2022.

Ninaipongeza Menejimenti ya Benki pamoja na wafanyakazi wote kwa kufanya kazi kwa bidii na kuwezesha kupatikana kwa mafanikio yaliyoainishwa katika Ripoti hii. Vilevile, ninawashukuru wenzangu, wajumbe wa Bodi kwa kutoa miongozo na uangalizi bora uliofanikisha utekelezaji wa malengo ya Benki. Leo hii ninasimama mbele yenu na kuwasilisha kwenu mafanikio ya Benki kwa mwaka 2022 yaliyotokana na kujitolea bila kuchoka na mchango wa kila mmoja wetu katika kufanikisha malengo ya Benki. Kwa dhati kabisa, ninawashukuru wateja wetu kwa kuendelea kuiunga mkono Benki yetu. Bila wao, Benki isingeweza kuyafikia mafanikio haya. Ninatumia pia fursa hii kuzishukuru taasisi zinazosimamia na kudhibiti sekta ya fedha ambazo ni pamoja na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Serikali na wadau wengine wote ambao kwa namna moja au nyingine wamekuwa wakiunga mkono na kutoa mwongozo kwa Benki. Kwa wanahisa wetu, ninawashukuru sana kwa kuendelea kuunga mkono na kuwezesha upatikanaji wa rasilimali mitaji ili kufanikisha malengo ya Benki.

**Mafanikio muhimu na maendeleo ya Benki kwa mwaka 2022 -**

Taarifa kamili ya mafanikio  inayo onyesha jinsi biashara ya Benki ilivyokua kwa mwaka 2022 imeandikwa katika kurasa za 55-95. Kwa sasa, ninawaomba tuambatane kuyapitia maendeleo muhimu ya Benki kama nilivyoainisha hapo chini. Vilevile, ninawasihi msome

Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ambayo ipo ndani ya kitabu hiki. Kwa kusoma Taarifa hiyo ya Mkurugenzi Mtendaji, mtapata kujua mafanikio ya biashara kwa undani na mipango yetu ya baadaye.

- Kipaumbele cha kimkakati cha Benki kinabaki kuwa ni kujitolea kukuza upatikanaji wa huduma jumuishi za kifedha. Ili kutimiza azma hiyo, Benki imekamilisha mchakato wa kutengamanisha huduma zetu na zile za wadau wengine muhimu katika utoaji wa huduma za kifedha kwa njia ya kidijitali kama vile kampuni za simu za mkononi na wengine.

- Tumepata mafanikio mazuri katika mchakato wa kuanzisha na kufikisha huduma zetu kwa njia ya Mawakala wa Benki (Mkombozi WAKALA), Kukusanya sadaka kwa njia ya kidijitali (SADAKA Digital) na kutoa huduma za fedha kwa njia ya mtandao (Internet Banking). Tumeimarisha chaneli yetu ya benki kwa njia ya Simu (Mobile Banking Channel) kwa kuzindua programu ya App. Wakati huohuo, wateja wetu wakipata huduma zetu kwa njia ya USSD.

- Tumekamilisha mipango ya kufungua matawi mapya Arusha na Mwanza ambayo yataanza kufanya kazi kabla ya mwisho wa robo tatu ya mwaka 2023. Tawi la Arusha lilifunguliwa na kuanza kutoa huduma tarehe 24 Mei, 2023.

- Tumekamilisha mipango ya kuhamisha Makao Makuu ya Benki na Tawi la Mt. Joseph kwenda Jengo jipya la Mt. Joseph. Jengo hili jipya ni muhimu na la kimkakati kwa sababu linasaidia kuimarisha muonekano wetu na kutoa picha ya ubora wa huduma zetu kwa wateja. Tutakamilisha mpango wa kuhamia jengo jipya katika robo ya tatu ya mwaka 2023.

- Tuliimarisha msingi wa rasilimali watu kwa kuajiri maofisa waandamizi sehemu za kimkakati hususani katika maeneo ya fedha na huduma za biashara. Tuliimarisha menejimenti za idara za mauzo na usimamizi wa uhusiano/huduma kati ya Benki na wateja ili kuendana na mipango yetu ya kukuza biashara na ubora wa huduma za Benki.

- Kwa ujumla, mipango yetu ya uimarishaji wa biashara na matarajio ya ukuaji wake yanaendelea kuleta matokeo chanya kama inavyoonyesha katika kuongezeka kwa idadi ya wateja, kuongezeka kwa mapato, usimamizi bora wa gharama za matumizi na ubora wa usimamizi wa vihatarishia hatari.

## Hali ya uchumi na soko kwa mwaka 2022

Shughuli za kiuchumi kwa mwaka 2022 zilidhoofishwa na changamoto za mnyororo wa usambazaji zilizotokana na Vita vya Ukraine, kurejea kwa UVIKO-19 na vikwazo vitokanavyo na mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo uwepo wa misingi thabiti ya kiuchumi, vimeiwezesha Tanzania kupunguza athari za UVIKO-19 na kuendelea kukua kwa uchumi. Hata hivyo, kasi ya ukuaji wa uchumi imepungua kutokana na athari za Vita vya Ukraine, hali isiyoridhisha ya kifedha duniani pamoja na kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia. Hata hivyo, kwa mwaka 2022 tumeshuhudia kufufuka kwa ukuaji wa uchumi ambapo sekta mbalimbali zimeanza kufanya vizuri na kurudi kuwa sawa na hali iliyokuwapo kabla ya UVIKO-19.

Katika nchi nyingi zilizoendelea kiuchumi, mfumuko wa bei ulipanda na kuvuka matarajio ya benki kuu za nchi husika kwa mwaka 2022. Kutokana na kupungua kwa vikwazo vya mnyororo wa usambazaji, kuanza kushuka kwa bei za bidhaa na utekelezaji wa sera za fedha zinazolenga kupunguza ongezeko la ukwasi kwenye uchumi, mfumuko wa bei ulianza kupungua kuelekea mwishoni mwa mwaka. Mfumuko wa bei kwa taifa ulikuwa asilimia 4.3 mwaka 2022 huku pato la Taifa likiongezeka kwa asilimia 4.7 kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.9 kwa mwaka 2021. Inatarajiwa kuwa pato la Taifa litaongezeka kwa asilimia 5.2 mwaka 2023 na 6.2 kwa mwaka 2024.

Utekelezaji wa sera za fedha ulifanikisha kudumisha uwepo wa ukwasi wa kutosha kwenye uchumi sambamba na malengo ya mfumuko wa bei. Kwa ujumla, sekta ya benki iliendelea kuwa na mtaji na ukwasi wa kutosha pamoja na kupata faida kwa mwaka mzima. Amana za wateja na mali za Benki ziliongezeka, sambamba na ubora wa mali zenyewe.

## Mpango mkakati wa mwaka 2022 mpaka 2023

Katika mpango wa muda wa kati, Benki inaendelea kuzingatia mipango mikakati ifuatayo ili kuongeza faida na kukua:

- Kutengeneza biashara yenye mwelekeo wa kidijitali kwa kutumia mawakala wa kibenki, kutoa huduma za benki kwa njia ya App, kutoa huduma za kibenki kwa njia ya mtandao na kutoa huduma za usimamizi wa fedha.

- Kupanua mtandao wa Benki kwa kufanya kazi na mawakala na kufungua matawi madogo madogo/vituo vya kutolea huduma.

- Kukuza biashara ya Benki kwa kuzingatia bidhaa maalumu zinazofaa kwa wateja maalumu. Katika hili, msisitizo wa kimkakati utawekwa katika kubadili muundo/mchanganyo wa amana kati ya Akaunti za Hundi na za Akiba kwa upande mmoja na Akaunti za Muda Maalumu kwa upande mwingine. Lengo la kuanzia mwaka mmoja hadi mitatu ni kwamba Akaunti za Hundi na za Akiba zifikie 70% ya amana zote huku Akaunti za Muda Maalumu zikifikia 30%.

- Kuimarisha Mfumo wa Mikopo (Chanzo, Usimamizi na Urekebishaji) ili kuwa na utaratibu mzuri wa mikopo utakaoleta ufanisi na faida kwa kipindi cha kuanzia mwaka mmoja hadi mitatu.

- Kuongeza nguvu katika kupunguza gharama za uendeshaji kwa lengo la kimkakati la kupata uwiano wa mapato na gharama wa 55% kwa muda wa kuanzia mwaka mmoja hadi mitatu.

- Kuboresha tija kwa wafanyakazi kwa kuwaongezea ujuzi na utekelezaji wa mfumo imara wa utendaji

- Kuimarisha mfumo wa huduma kwa wateja ili kuboresha huduma zitolewazo na Benki.

- Kuimarisha ubunifu na uwekezaji katika teknolojia ili kuboresha huduma zetu. Hili ni pamoja na kuwekeza katika kubadili mfumo wa kiteknolojia unaosimamia huduma zetu za kibenki.

## Nyaraka za Mkutano Mkuu wa Mwaka

Nyaraka za Mkutano Mkuu wa Mwaka ambazo kila mwanahisa amepewa ni pamoja na Taarifa ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha kwa mwaka unaoishia Desemba 2022. Hizi zimekabidhiwa kwenu rasmi ili zijadiliwe na kupitishwa. Wanahisa wote mnakaribishwa kushiriki katika majadiliano haya na kutoa michango yenu muhimu ili kwa pamoja tujenge Benki inayokuwa kwa kasi zaidi na yenye ukuaji endelevu.

Kwa niaba ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, ninawashukuru kwa mara nyingine kwa kushiriki katika mkutano huu muhimu na kuendelea kuiunga mkono Benki yenu. Ninawatakia mafanikio mema ya Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 14.

Asanteni na Mungu awabariki,

**GASPER CASMIR NJUU**
**MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI**
**Julai 29, 2023**

# TAARIFA YA MKURUGENZI MTENDAJI

**Wapendwa Wanahisa,**

Ninayo furaha kuthibitisha kwamba mwaka 2022 ulikuwa mzuri kwa Benki yetu kwa kuangalia vigezo kadhaa vinavyotumika kupima utendaji. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kuendelea kuiweka Benki katika nafasi ya kimkakati ili iweze kufanikiwa kupata rasilimali muhimu na miundombinu. Benki iliendelea kustahimili changamoto mbalimbali na kuonesha matokeo mazuri sambamba na vipaumbele vya kimkakati, kuboresha ufanisi na ubora wa mikopo, kuimarisha mizania na kuvuna mapato mazuri.

Tumepiga hatua nzuri katika safari yetu ya mabadiliko kimkakati na matokeo yake yako wazi. Haya ni matokeo ya miaka mingi ya uthabiti na nidhamu katika usimamizi wa gharama, maboresho ya mikopo, mpangilio wa huduma na mchakato pamoja na uwekezaji kwa rasilimali watu na teknolojia. Baada ya kujenga msingi imara kupitia utekelezaji wa mkakati wetu wa "Mageuzi na Maboresho" (2020-2023), tuliongeza kasi ya utekelezaji ili kuimarisha mafanikio tuliyoyapata na kuwasilisha malengo muhimu ya mwaka 2022.

Tumekuwa na ufanisi zaidi. Tumeshughulikia changamoto za mikopo na utendaji wa zamani. Tumeimarisha mtaji na kutoa huduma nyingi zaidi kwa njia za kidijitali. Matokeo ya haya yote ni Benki kupata ongezeko kubwa zaidi la faida ambayo haijawahi kutokea katika historia yake. Wanahisa wanao mchango mkubwa sana katika mafanikio haya kwa sababu ndiyo waliojitolea katika safari ya kuongeza mtaji wa Benki. Kwa miaka mitatu iliyopita, Benki imepunguza kiasi cha hasara limbikizi kutoka Shilingi bilioni 11.3 mwaka 2019 hadi Shilingi bilioni 1.49 hivi sasa. Fedha hizi zimesaidia sana kuongeza mtaji wa Benki. Ni matarajio yetu kwamba tutaukamilisha mkakati wetu mwaka 2023, na kuanza kupata faida limbikizi, hatua itakayotuwezesha kujenga uwezo wa kutoa gawio kwa wanahisa wetu. Tunawashukuru wanahisa wetu na wateja wetu kwa kuiamini Benki yetu na kuipatia nafasi ya kuwahudumia. Kwa moyo wa dhati kabisa, ninasema ASANTENI SANA.

## Matokeo ya Vipimo Muhimu vya Fedha

## Muhtasari wa Vipimo Muhimu vya Utendaji (Namba kamili kwa milioni za TZS)

| SN | Kipimo cha Fedha | 31/12/2022 | 31/12/2021 (Imerudiwa*) | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 25,666 | 22,076 | 3,590 |
| 2 | Faida (Hasara)* itokanayo na Marekebisho ya mikopo | 1,021 | (2,758) | 3,779 |
| 3 | Ada na Kamisheni | 4,673 | 4,403 | 270 |
| 4 | Gharama za Riba | (7,320) | (8,787) | 1,467 |
| 5 | Gharama za Uendeshaji | (15,951) | (15,662) | (289) |
| 6 | Tengo kwa ajili ya Mikopo Chechefu | (2,944) | (1,979) | (965) |
| 7 | Faida ya Uendeshaji | 5,145 | (2,707) | 7,852 |
| 8 | Tengo la Kodi ya Mapato | 476 | 847 | (371) |
| 9 | Faida Halisi baada ya Kodi ya Mapato | 5,621 | (1,860) | 7,481 |
| 10 | Mapato mengine yaliyojumuishwa | 1,178 | (37) | 1,215 |
| 11 | Jumla ya Faida iliyojumuishwa | 6,799 | (1,897) | 8,696 |
| 12 | Mikopo Halisi iliyopo | 115,039 | 106,860 | 8,179 |
| 13 | Amana za Serikali | 43,208 | 42,669 | 539 |
| 14 | Amana za Wateja | 184,579 | 181,513 | 3,066 |
| 15 | Mapato Yaliyobakizwa | (1,499) | (9,056) | 7,557 |
| 16 | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 9% | 9% | - |
| 17 | Uwiano wa Gharama za Uendeshaji na Mapato Ghafi | 62% | 90% | 28% |
| 18 | Uwiano wa Utoshelevu wa Mtaji (CAR) | 13.05% | 9% | 4% |

**Inatokana na marekebisho ya kimahesabu wakati wa kufanya marekebisho ya mali za kifedha kutokana na mabadiliko ya mbinu za kupiga hesabu za riba ili kuendana na Kanuni za Kumlinda Mlaji wa Huduma za Mwaka 2019 kutoka ile [mbinu] ya SAWIA na sasa tunatumia ya KUPUNGUZA.*

### Mapato – Kukuza/Kuimarisha Mali ziletazo mapato

Kiwango cha mikopo kiliongezeka kwa TZS bilioni 8.17 na kufika TZS bilioni 115.03 mwaka 2022 ikilinganishwa na TZS bilioni 106.86 kwa mwaka 2021. Ongezeko hili lilitokana na juhudi za kuongeza mikopo midogo midogo ambayo iliwezesha kuongezeka kwa Mikopo ya Vikundi vya Pamoja, yaani, Solidarity Group Loans (SGL) kuongezeka kwa jumla ya TZS bilioni 2.10 na kufikia TZS bilioni 5.73 ikilinganishwa na TZS bilioni 3.64 za mwaka 2021. Pamoja na kwamba mapato ya Benki kwa kiasi kikubwa hutokana na Mapato ya Riba, tunaendelea na juhudi za kukuza mapato yasiyo ya riba ili kuimarisha tija na ufanisi wa biashara kwa ujumla.

### Gharama – Kuimarisha utamaduni wa nidhamu ya matumizi

Nidhamu ya matumizi ndiyo siri ya mafanikio ya kuleta faida kwa wanahisa kwa sababu kwa kadiri tunavyotumia kiasi kidogo ili kuzalisha Shilingi Moja ya Mapato ndivyo hivyo matokeo ya fedha yanavyokuwa mazuri. Kwa hiyo, tangu mwanzo, tulifanya uamuzi mgumu wa kubana matumizi. Tumefanikiwa kupunguza matumizi na matokeo yake mwaka 2022, tumeboresha uwiano wa ufanisi na kufikia asilimia 62 (kutoka asilimia 90 mwaka 2021). Tunaendelea kutafuta mbinu za kuboresha zaidi ufanisi wetu bila kuathiri mipango ya kukuza mapato ili tufikie viwango vinavyopendekezwa na Benki Kuu ambavyo ni kuwa na uwiano wa 55% wa gharama za uendeshaji ikilinganishwa na mapato ghafi. Tukifikia hatua hiyo ndipo tutakaporuhusiwa kutoa gawio kwa wanahisa kwa mujibu wa kanuni za Benki Kuu ya Tanzania.

### Faida ya Uendeshaji – Kujenga Uendeshaji Wenye Tija

Faida yetu ya uendeshaji imeongezeka kutokana na nidhamu yetu ya matumizi. Pamoja na kuwa tumeendelea kuwekeza kiasi kikubwa cha fedha katika miundo msingi na rasilimali za uendeshaji mwaka hadi mwaka, gharama zetu za uendeshaji zimepungua kwa asilimia nane (8) na kufikia TZS bilioni 15.90 mwaka 2022 kutoka TZS bilioni 17.28 mwaka 2019. Jambo hili ni muhimu wakati huu tunapotafuta mbinu za kupanua vyanzo vyetu vya mapato ili kuchochea ongezeko la faida na azma yetu ya kuikuza zaidi Benki.

## Ukwasi – Ukwasi wa kutosha

Mizania ya Benki inaonyesha uwepo wa ukwasi mzuri na mtaji wa kutosha. Jumla ya mali ziliongezeka kwa TZS bilioni 11 na kufikia TZS bilioni 221.72 (sawa na ongezeko la asilimia tano) kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na TZS bilioni 210.72 mwaka 2021. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa Amana za Wateja jambo ambalo linaonyesha wateja wanayo Imani kubwa na Benki yetu. Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Amana ni asilimia 63. Hili linatoa nafasi ya kutosha kwetu kuendelea na shughuli zetu za kutoa mikopo, hususani kwa eneo la soko linaloendana na dira na dhima ya Benki. Mali za Benki ambazo zinaweza kubadilishwa kuwa fedha kwa muda mfupi zimeongezeka kutokana na uamuzi wetu wa kuongeza umakini katika utoaji mikopo. Uwekezaji wetu katika Dhamana (Dhamana za Serikali za muda mrefu na muda mfupi) umeongezeka kwa TZS milioni 539 na kufikia TZS bilioni 43.2**.** Vilevile, Amana zetu zilizo katika benki nyingine na taasisi za fedha zimeongezeka kwa TZS milioni 996 na kufikia TZS bilioni 24.13. Fedha hizi ni ishara ya uwepo wa ukwasi wa kutosha katika Mizania ya Benki yetu.

## Maboresho ya vipimo vya ubora wa mali

Moja kati ya malengo yetu ya kimkakati ni kuendelea kutafuta ufumbuzi wa mikopo chechefu iliyotolewa zamani ili kuboresha utolewaji wa mikopo. Tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika haya yote mawili. Kiwango cha Mikopo Chechefu kimepungua na kufikia TZS bilioni 11.47 kutoka TZS bilioni 14.01 mwaka 2021. Hata hivyo, uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi bado ni asilimia tisa (9) kama ilivyokuwa mwaka uliotangulia. Hii inatokana na kupungua kwa uwiano wa jumla ya mikopo iliyotolewa. Uwiano huu uko juu ya kiwango kinachopendekezwa na Benki Kuu ya Tanzania cha asilimia tano (5). Malengo yetu ni kupunguza zaidi uwiano huu kwa mwaka 2023 ili hatimaye tufikie kiwango kinachopendekezwa na Benki Kuu.

## Mtaji unaoendana na mipaka ya udhibiti

Uwezo wa mizania ya benki kuhimili changamoto za kifedha hupimwa kwa tumia viwango vya Uwiano wa Utoshelevu wa Mtaji (CAR). Kuna viwango vya mtaji Kundi la kwanza (1) na za Kundi la pili (2) vinavyojulikana kitaalam kama Tier 1 na Tier 2. Kwa Tier 1, CAR inapaswa isiwe chini ya 12.5%

na zile za Tier 2 zinapaswa zisiwe chini ya 14.5%. Kwa mwaka 2022, CAR ya Benki yetu kwa Tier 1 ilikuwa 13.03% na Tier 2 ilikuwa 14.8%, vyote vilikidhi viwango vinavyopendekezwa na Benki Kuu ya Tanzania. Kuboreshwa kwa CAR kunatokana na kuongezeka kwa faida baada ya kodi ambayo ilipanda na kufikia TZS bilioni 6.79 pamoja na kupatikana kwa deni la kusaidia kuongeza mtaji la Tier 2 wa jumla ya TZS bilioni 2.7 Januari 2022. Hata hivyo, kiwango hiki cha mtaji ni kidogo kuweza kukidhi matamanio ya wawekezaji ya ukuaji wa benki hususani kupanua huduma za Benki na kukuza urari wa biashara.

### Huduma kwa Wateja

Tunanuia kuwa Benki Namba Moja nchini katika kutoa huduma bora kwa wateja. Tunaendelea kuboresha huduma zetu kwa kupeleka huduma zetu karibu na wateja wetu na kuboresha kasi ya utoaji huduma zenyewe. Mpaka sasa tumeimarisha utoaji wa huduma zetu kwa wateja kwa kuweka mfumo thabiti wa kufuatilia malalamiko yao na namna ya kuyatatua.

### Teknolojia na mipango ya upanuzi wa biashara

Mabadiliko ya kila mara ya mazingira shindani ya uendeshaji yanatubidi kufanya uwekezaji wa mara kwa mara katika teknolojia ili kuboresha ufanisi na huduma kwa wateja. Kutokana na hali hii, tumewekeza katika kutoa huduma kidijitali ili kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za Benki. Tunatoa huduma zetu kwa kushirikiana na Mawakala (ambapo mpaka Mei, 2023 tumesajili mawakala 476), kutoa huduma za kibenki kwa njia ya mtandao (ambapo mpaka Mei 2023 tumesajili wateja zaidi ya 600 wanaopata huduma zetu kwa njia ya mtandao, yaani, internet), kutoa huduma ya ukusanyaji sadaka kwa makanisa – SADAKA Digital (ambapo mpaka Mei, 2023 tumeziunganisha Parokia zaidi ya 170 kwenye huduma hii). Hivi sasa tunakamilisha ujenzi wa mfumo wa Malipo kwa kutumia mfumo wa kieletroniki wa serikali (Government e-Payment Gateway) ambao utazinduliwa mwezi Julai, 2023.

Tumefungua tawi letu la 12 kule Jijini Arusha tarehe 24 Mei, 2023 ambalo linapatikana katika jengo la PSSSF, Kiwanja Namba 15, Kizimba Namba 2 Barabara ya Nyerere. Kufunguliwa kwa tawi hili ni hatua muhimu katika safari yetu ya upanuzi wa huduma zetu. Arusha ni muhimu sana kwa biashara ya Benki yetu. Tunaamini kwamba Arusha kuna fursa nyingi

ambazo bado hazijatumika kwa aina ya wateja tunaowatarajia ambao ni Kanisa na taasisi zake pamoja na sekta nyingine za uchumi kama vile utalii na mapumziko. Tunaendelea na juhudi za kufungua matawi madogo mawili kabla ya mwaka 2023 kumalizika, moja litakuwa Jijini Mwanza eneo la Hospitali ya Bugando na jingine litakuwa Jijini Mbeya. Ufunguzi wa matawi haya utaisaidia Benki kutimiza mpango wake wa ukuaji na faida endelevu.

### Tuendako

Hali yetu ya uendeshaji na mazingira yake yanatubidi kutoa kipaumbele kwa hatua ambazo ni muhimu kwa kuiendeleza Benki. Tutaendelea kufanya uamuzi wa kuwajibika katika ugawaji wa rasilimali ili kutimiza azma ya kukuza biashara. Tutaandaa malengo yetu ili yaendane na muktadha wetu wenyewe kisha tutayaoanisha na mpango wetu wa biashara na mazingira yetu.

Ninajisikia fahari kupata nafasi ya kuongoza taasisi hii wakati huu inapopitia mabadiliko sambamba na ajenda yake ya kimkakati ya mabadiliko na ukuaji. Ninajivunia michango ya wafanyakazi, wanahisa, wajumbe wa bodi, jamii, Serikali, wasimamizi na wadhibiti wa sekta na wengine wengi katika kufanikisha juhudi zetu za kufanikisha dira ya Benki. Tumeamua kuibadilisha Benki ya Biashara Mkombozi kwa faida ya wadau wote.

**Respige Kimati.**

**Mkurugenzi Mtendaji.**

**Julai 29, 2023**

## AJENDA YA 3

# KUTHIBITISHA DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WANAHISA WA 13 ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA UBUNGO PLAZA JULAI 30, 2022

### WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Gasper Casmir Njuu | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhashamu Baba Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya | - | Mjumbe |
| 3. | Bi. Uphoo Swai | - | Mjumbe |
| 4. | Bw. Robert Mtendamema | - | Mjumbe |
| 5. | Bw. Benedict Sudi Wariasanga | - | Mjumbe |
| 6. | Bw. Martin Mdoe | - | Mjumbe |
| 7. | Bw. Respige Onesmo Kimati | - | Mkurugenzi Mtendaji |
| 8. | Bw. Osward Mpangala | - | Meneja wa Huduma za Sheria |

### UDHURU

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Padre Dkt. Charles. Kitima | - | Mjumbe |

### WAGENI WAALIKWA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Elibariki Fanuel Mkireni | - | Mwakilishi wa Ernst & Young |
| 2. | Bw. Meckland Edson | - | Mwakilishi wa Soko la Hisa la Dar es Salaam |
| 3. | Bi. Aisha M. Mbilikira | - | Mwakilishi kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) |

## WANAHISA

| Na. | JINA | HALI YAKE |
|---|---|---|
| 1 | ABEL BERA SEBASTIAN | Anatambulika |
| 2 | ABEL KUSIGA | Anatambulika |
| 3 | ADELLA F. KAVISHE | Anatambulika |
| 4 | ADRIAN J MAKELELE | Anatambulika |
| 5 | AEMP/SCHOOL-DIOCESE OF GEITA | Anatambulika |
| 6 | AFROKIA C KWEKA | Anatambulika |
| 7 | AGATHA E. MAYE | Anatambulika |
| 8 | AGNESS JOHN KIWIA | Anatambulika |
| 9 | ALBERT H. MILANZI | Anatambulika |
| 10 | ALCP/OSS AFRICA PROVINCE | Anatambulika |
| 11 | ALEX ATHUNAS | Anatambulika |
| 12 | ALEX STEPHAN KASILO | Anatambulika |
| 13 | ALEXUS C. MUTASINGWA | Anatambulika |
| 14 | ALFRED B. MILLEMBE | Anatambulika |
| 15 | ALFRED MATIKO | Anatambulika |
| 16 | ALINANINE MWAKILABA | Anatambulika |
| 17 | ALOYS B. MWACHA | Anatambulika |
| 18 | ALOYS D. SHUKURU | Anatambulika |
| 19 | ANASTASIA D. MASHUBU | Anatambulika |
| 20 | ANDREA M. MGAYA | Anatambulika |
| 21 | ANGELA J. KYAKULA | Anatambulika |
| 22 | ANSGAR ROBERT MAPUNDA | Anatambulika |
| 23 | ANTHONY J. LUBUVA | Anatambulika |
| 24 | APOLINARY B. MWARABU | Anatambulika |
| 25 | ARCHDIOCESE OF ARUSHA | Anatambulika |
| 26 | ARCHDIOCESE OF DAR ES SALAAM | Anatambulika |
| 27 | ARCHDIOCESE OF SONGEA | Anatambulika |
| 28 | ARCHIDIOCESE OF ARUSHA | Anatambulika |
| 29 | ARTHUR O. GAMA | Anatambulika |
| 30 | ASSENGA SCAROLI | Anatambulika |
| 31 | ASUNTA VENANCE IKONKO | Anatambulika |
| 32 | AUGUSTINE R. KASHULI | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 33 | B. E. TEMU | Anatambulika |
| 34 | BAHATI ADEN KAJELA | Anatambulika |
| 35 | BEATA M. NGANDAKU | Anatambulika |
| 36 | BERNADETHA P. MASANJA | Anatambulika |
| 37 | BERTOLD T. NJAWIKE | Anatambulika |
| 38 | BIHAWANA SEMINARY | Anatambulika |
| 39 | BINGILEKI F BINGILEKI | Anatambulika |
| 40 | BISHOP BEATUS KINYAIYA | Anatambulika |
| 41 | BUGANDO MEDICAL CENTRE | Anatambulika |
| 42 | CALIST A. CHUWA | Anatambulika |
| 43 | CALISTUS PHILIP ASSENGA | Anatambulika |
| 44 | CATHERINE M. VINGILLAH | Anatambulika |
| 45 | CATHERINE MWIDETE | Anatambulika |
| 46 | CATHOLIC DIOCESE LINDI | Anatambulika |
| 47 | CATHOLIC DIOCESE OF IFAKARA | Anatambulika |
| 48 | CATHOLIC DIOCESE OF KAHAMA | Anatambulika |
| 49 | CATHOLIC DIOCESE OF MBULU | Anatambulika |
| 50 | CATHOLIC DIOCESE OF MOROGORO | Anatambulika |
| 51 | CATHOLIC DIOCESE OF MOSHI | Anatambulika |
| 52 | CELINA D. MREFU | Anatambulika |
| 53 | CHARLES LUBAWA | Anatambulika |
| 54 | CHRISTIAN ALOYCE | Anatambulika |
| 55 | CHRISTINA C. MCHAMI | Anatambulika |
| 56 | CHRISTINA FABIAN KAPEMBE | Anatambulika |
| 57 | CLAUDI C. MFUNGO | Anatambulika |
| 58 | CLEVINA TIBAMANYA | Anatambulika |
| 59 | CONSAVIUS LWILLA | Anatambulika |
| 60 | CONSOLATA ALBERT BEBWA | Anatambulika |
| 61 | CUTHBERT KARLIHANGA | Anatambulika |
| 62 | DANIEL M. UBALANJE | Anatambulika |
| 63 | DANIEL MEEHAN KINDAGARTEN | Anatambulika |
| 64 | DAYANA B. MGUMBA | Anatambulika |
| 65 | DEVINA MATOLA | Anatambulika |
| 66 | DEVOTHA P. CHAMWALI | Anatambulika |
| 67 | DINA H MBUBA | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 68 | DIOCESE OF BUKOBA | Anatambulika |
| 69 | DIOCESE OF BUNDA | Anatambulika |
| 70 | DIOCESE OF DODOMA ITF: SECRETARIAT OF CATHOLIC DIOCESE OF DODOMA | Anatambulika |
| 71 | DIOCESE OF GEITA | Anatambulika |
| 72 | DIOCESE OF GEITA ITF: OLD AGE | Anatambulika |
| 73 | DIOCESE OF GEITA ITF: OLD AGE-DIOCESE OF GEITA | Anatambulika |
| 74 | DIOCESE OF IRINGA | Anatambulika |
| 75 | DIOCESE OF KAYANGA, | Anatambulika |
| 76 | DIOCESE OF KIGOMA | Anatambulika |
| 77 | DIOCESE OF KIGOMA ITF: DIOCESE OF KIGO-MA | Anatambulika |
| 78 | DIOCESE OF KONDOA | Anatambulika |
| 79 | DIOCESE OF LINDI | Anatambulika |
| 80 | DIOCESE OF MAHENGE (DIOCESE) | Anatambulika |
| 81 | DIOCESE OF MBINGA | Anatambulika |
| 82 | DIOCESE OF MPANDA | Anatambulika |
| 83 | DIOCESE OF MTWARA | Anatambulika |
| 84 | DIOCESE OF MUSOMA | Anatambulika |
| 85 | DIOCESE OF MWANZA | Anatambulika |
| 86 | DIOCESE OF NJOMBE | Anatambulika |
| 87 | DIOCESE OF RULENGE | Anatambulika |
| 88 | DIOCESE OF RULENGE NGARA | Anatambulika |
| 89 | DIOCESE OF RULENGE-NGARA ITF: RULENGE DIOCESE PRIEST FUND | Anatambulika |
| 90 | DIOCESE OF SINGIDA | Anatambulika |
| 91 | DIOCESE OF SUMBAWANGA | Anatambulika |
| 92 | DIOCESE OF SUMBAWANGA ITF: IDARA YA AFYA JIMBO | Anatambulika |
| 93 | DIOCESE OF TANGA | Anatambulika |
| 94 | DIOCESE OF TUNDURU – MASASI | Anatambulika |
| 95 | DIOCESE OF ZANZIBAR | Anatambulika |
| 96 | DISMAS ISSA MLUNGAMO | Anatambulika |
| 97 | DISMASIA E. LYANGANI | Anatambulika |
| 98 | DONATI P. KULENGA | Anatambulika |
| 99 | DOROTHY MWAISALA | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 100 | DR. MAGOKE GODFREY | Anatambulika |
| 101 | EDWARD M. MWAIBAMBE | Anatambulika |
| 102 | EDWARDINA NGAIZA | Anatambulika |
| 103 | EDWINA A. LUPEMBE | Anatambulika |
| 104 | ELIAS A MMAIZI | Anatambulika |
| 105 | EMELDA CHARLES MWENDA | Anatambulika |
| 106 | EMERENCIANA L. UTOUL | Anatambulika |
| 107 | EMIL G. TESHA | Anatambulika |
| 108 | EMMANUEL KULANGESIWA | Anatambulika |
| 109 | EMMY MAGENI | Anatambulika |
| 110 | ENGTRAUDA P. MUMBA | Anatambulika |
| 113 | ENOCK PH KIKOTI | Anatambulika |
| 114 | ERICK MWARABU K | Anatambulika |
| 115 | ERNEST P. LYAMANYELE | Anatambulika |
| 116 | ESSAYAS THOMAS MGENDERA | Anatambulika |
| 117 | ESTHER M. MHANGA | Anatambulika |
| 118 | EUPTROPEA H. MARO | Anatambulika |
| 119 | EVA JOHN MKUNDI | Anatambulika |
| 120 | EVARIST A. MINANI | Anatambulika |
| 121 | EWALD N. MREMA | Anatambulika |
| 122 | EXPEDITO D SIMMON | Anatambulika |
| 123 | FABIAN LAURENT | Anatambulika |
| 124 | FARAJA MASSAWA | Anatambulika |
| 125 | FARIJIKA RWAMASHONGA | Anatambulika |
| 126 | FAUSTER FAUSTIN KIWIA | Anatambulika |
| 127 | FAUSTUS G. RUGONDA | Anatambulika |
| 128 | FLORA MBINGA | Anatambulika |
| 129 | FORTUNATA CHAGU | Anatambulika |
| 130 | GENEROSA JOSEPH RUTAIHWA | Anatambulika |
| 131 | GERVAS J. KAVISHE | Anatambulika |
| 132 | GERVAS L. MBILINYI | Anatambulika |
| 133 | GESMIRA SHANGWA | Anatambulika |
| 134 | GISLA KASIANZULU | Anatambulika |
| 135 | GODFREY MANDONDA KIBANDA | Anatambulika |
| 136 | GRACE DAVID MUSHI | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 137 | HENRY J. MBOYA | Anatambulika |
| 138 | HUGO EUGEN SHIRIMA | Anatambulika |
| 139 | HUSNA HAJI KAVISHE | Anatambulika |
| 140 | IJAGALA TRUST CO.LTD | Anatambulika |
| 141 | IMMACULATA D. MUTAISHAIRWA | Anatambulika |
| 142 | INNOCENT MARCO KAPALALE | Anatambulika |
| 143 | ITCL | Anatambulika |
| 144 | JANEMARY RUTAHOILE | Anatambulika |
| 145 | JANEVUITSA MWANYIKA | Anatambulika |
| 146 | JANUARY MARIA | Anatambulika |
| 147 | JAPHET TINDWA | Anatambulika |
| 148 | JASTAS S. MKORONGO | Anatambulika |
| 149 | JERRY B. MWASA | Anatambulika |
| 150 | JESCA JOEL KABALIBAL | Anatambulika |
| 151 | JIMBO KATOLIKI MOSHI | Anatambulika |
| 152 | JOAN MSUYA | Anatambulika |
| 153 | JOHANES E. MACHUMU | Anatambulika |
| 154 | JOHN EWALO MOSHY | Anatambulika |
| 155 | JOHN M BIZONGWAKO | Anatambulika |
| 156 | JOHN MWANYINGILI MWALYANGO | Anatambulika |
| 157 | JOSEPH J KESSY | Anatambulika |
| 158 | JOSEPH J.H. KIJERUDA | Anatambulika |
| 159 | JOSEPHINA P. MBILINYI | Anatambulika |
| 160 | JOSEPHINE MUHULA | Anatambulika |
| 161 | JOVINA KIPONGO | Anatambulika |
| 162 | JUDITH MKOBA | Anatambulika |
| 163 | JULIUS MBAWALA | Anatambulika |
| 164 | JUMUIYA MT. CECILIA | Anatambulika |
| 165 | JUMUIYA MT. CECILIA MLANDEGE | Anatambulika |
| 166 | JUMUIYA YA BIKIRA MARIA | Anatambulika |
| 167 | KARISTO ALFRED MFALAMAGOHA | Anatambulika |
| 168 | KAYANGA CATHOLIC DIOCESE | Anatambulika |
| 169 | KELVIN LUSEKELO MSUSI | Anatambulika |
| 170 | KIMARA CATHOLIC CHURCH | Anatambulika |
| 171 | KOLETHA MWALUGENGE | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 172 | KONDOA CATHOLIC DIOCESE | Anatambulika |
| 173 | KWAYA YA UPENDO | Anatambulika |
| 174 | LAMBERTHA NYASINT MAHAI | Anatambulika |
| 175 | LAURENT KEWE | Anatambulika |
| 176 | LAWRENTIA MALWA MAYOLI | Anatambulika |
| 177 | LEONARDINA I. MAPUNDA | Anatambulika |
| 178 | LETICIA CHAMBILA | Anatambulika |
| 179 | LEY CAMILIAN FAMILY | Anatambulika |
| 180 | LIGHTNESS MBUTA | Anatambulika |
| 181 | LINA L. MISANA | Anatambulika |
| 182 | LONGINUS BANKYANULE | Anatambulika |
| 183 | LOUIS SEVELIN KESSY | Anatambulika |
| 184 | LUCIANA A MADUGA | Anatambulika |
| 185 | LUCY GEORGE MAYAO | Anatambulika |
| 186 | LUTIGARDA L. RWEZAULA | Anatambulika |
| 187 | MAENDELEO GROUP | Anatambulika |
| 188 | MAKIANA A. NDONJEKWA | Anatambulika |
| 189 | MAKUBURI PARISHI | Anatambulika |
| 190 | MAKUBURI PARISHI-KWAYA YA MT. KIZITO | Anatambulika |
| 191 | MAKUBURI PARISHI-MT. THERESIA WA MTO-TO YESU | Anatambulika |
| 192 | MALYON WOSS SIGALA | Anatambulika |
| 193 | MARCELLA MARTIN KOMBA | Anatambulika |
| 194 | MARCELLINO X. KAYOMBO | Anatambulika |
| 195 | MARCO J. MWENDA | Anatambulika |
| 196 | MARIA DIMOSSO | Anatambulika |
| 197 | MARIA FELIX SILAYO | Anatambulika |
| 198 | MARIA ROMANI | Anatambulika |
| 200 | MARIA WA LURD | Anatambulika |
| 201 | MARIAB. MGUMBA | Anatambulika |
| 202 | MARTIN R. SINGWA | Anatambulika |
| 203 | MARY K. NGOLE | Anatambulika |
| 204 | MARY KIWIA | Anatambulika |
| 205 | MARY MAHUCHO MSEMWA | Anatambulika |
| 206 | MATHIAS C. MKULA | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 207 | MATHIAS LAURENT | Anatambulika |
| 208 | MATHIAS MUJUAMUNGU | Anatambulika |
| 209 | MELCHIOR NJIGE | Anatambulika |
| 210 | MESHACK CHACHA | Anatambulika |
| 211 | METHOD KAMALA | Anatambulika |
| 212 | MGANDA V. OSCAR | Anatambulika |
| 213 | MICHAEL KASHINDYE | Anatambulika |
| 214 | MICHAEL YEREMIA LUVANGA | Anatambulika |
| 215 | MODESTA M. JENGO | Anatambulika |
| 216 | MONICA ELIA | Anatambulika |
| 217 | MOYO MT. WA YESU | Anatambulika |
| 218 | MT. AGATHA MSASANI | Anatambulika |
| 219 | MWISHE M. LAURENT | Anatambulika |
| 220 | NATALIA H. SHIRIMA | Anatambulika |
| 221 | NEEMA MELCHIOR NUNGU | Anatambulika |
| 222 | NEMES THOBIAS MKUDE | Anatambulika |
| 223 | NICHOLAUS MALANDO | Anatambulika |
| 224 | NICODEMAS T. KANJE | Anatambulika |
| 225 | NICODEMUS JOSEPH KISHEA | Anatambulika |
| 226 | OLIVER A. KULANGISIWA | Anatambulika |
| 227 | OLIVER PETER | Anatambulika |
| 228 | OLYMPIA ODILLO | Anatambulika |
| 229 | ONESMO R. NDAKI | Anatambulika |
| 230 | OTHMAN MAALIM ZARALI | Anatambulika |
| 231 | OZANA MWANICHETA KINYONTO | Anatambulika |
| 232 | PASCHAL MALIFEDHA KANYALA | Anatambulika |
| 233 | PATRICK N. SHIRIMA | Anatambulika |
| 234 | PENINA OSWARD MARWA | Anatambulika |
| 235 | PERAMIHO SEMINARY | Anatambulika |
| 236 | PETER A. ALLOO | Anatambulika |
| 237 | PETER J KESSY | Anatambulika |
| 238 | PETER PAUL | Anatambulika |
| 239 | PILIKA PRISILA RASHID | Anatambulika |
| 240 | PRIMITIVA P. KAMUGISHA | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 241 | PRISCILLA G. MSAFIRI | Anatambulika |
| 242 | PROF.MARCELLINA MVULA CHIJORIGA | Anatambulika |
| 243 | PULKERIA EMILY | Anatambulika |
| 244 | RAHELI MOSHI | Anatambulika |
| 245 | RAYMOND MSOMA | Anatambulika |
| 246 | REGINA JOEL KABALIBAL | Anatambulika |
| 247 | REHEMA LUBAWA | Anatambulika |
| 248 | REVOCATUS R. MSHEMA | Anatambulika |
| 249 | ROSALIA DIDAS WATUGULU | Anatambulika |
| 250 | ROSE B. MBUTA | Anatambulika |
| 251 | RULENGE - NGARA CATHOLIC DIOCESE | Anatambulika |
| 253 | SALMA MWASA | Anatambulika |
| 254 | SALUSTIAN THOBIAS NKOLA | Anatambulika |
| 255 | SALVATORIAN SISTERS | Anatambulika |
| 256 | SCHOLASTICA J. NTIRUKA | Anatambulika |
| 257 | SCHOLASTICA MATEI | Anatambulika |
| 258 | SECHELALI J. HOKORORO | Anatambulika |
| 259 | SELINA MLINGI | Anatambulika |
| 260 | SEVERINI KASMIRI NYEHO | Anatambulika |
| 261 | SHEDIRICK M. KISINGA | Anatambulika |
| 262 | SIMON MRINA | Anatambulika |
| 263 | SRS.OF ST. GEMMA-DODOMA | Anatambulika |
| 264 | ST. AUGUSTINE UNIVERSITY OF TANZANIA -MWANZA | Anatambulika |
| 265 | ST. JOHN BOSCO PARISH | Anatambulika |
| 266 | STELLA P. BUNDALA | Anatambulika |
| 267 | STELLAH L. BANKYANULE | Anatambulika |
| 268 | TANZANIA EPISCAPAL CONFERENCE (TEC) | Anatambulika |
| 269 | TEC | Anatambulika |
| 270 | THE REGISTERED TRUSTEES OF THE ROMAN CATHOLIC DIOCESE OF KIGOMA | Anatambulika |
| 271 | THEODORA SABINUS | Anatambulika |
| 272 | THERESIA ZAWADI NKUNJA | Anatambulika |
| 273 | THOMAS JULIUS NG'WALA | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 274 | TRUSTEES OF THE CATHOLIC ARCHDIOCESE OF TABORA | Anatambulika |
| 275 | TUPENDANE WOMEN | Anatambulika |
| 276 | TUPENDANE WOMEN | Anatambulika |
| 277 | UFUMWA SACCOSS LTD | Anatambulika |
| 278 | UNIVERSITY CATHOLIC COMM. | Anatambulika |
| 279 | UWAMBE SACCOS LTD | Anatambulika |
| 280 | VALENCE A. KATUMWA | Anatambulika |
| 281 | VENANCE SANGAWE | Anatambulika |
| 282 | VERDIANA MARGAI | Anatambulika |
| 284 | VERONICA KIIZA | Anatambulika |
| 285 | VERONICA LUCAS HONERO | Anatambulika |
| 286 | VERONICA R. KANWERA | Anatambulika |
| 287 | VIANEY P. LINGA | Anatambulika |
| 288 | VICKY MARINO LAFFA | Anatambulika |
| 289 | VICTORIA A. GANAI | Anatambulika |
| 290 | VICTORIA E LUKUMBA | Anatambulika |
| 291 | VICTORIA LUKWEMBA | Anatambulika |
| 292 | VICTORIA S. KISANJI | Anatambulika |
| 293 | VICTORIA STEPHEN MAUI | Anatambulika |
| 294 | WENSE L. ULIMALI | Anatambulika |
| 295 | WILLIAM ISRAEL KITALI | Anatambulika |
| 296 | WINIFRIDA P. KAMUGISHA | Anatambulika |
| 297 | WITNES A. MAZUBU | Anatambulika |
| 298 | YAVAN SHEDRACK FOYA | Anatambulika |
| 299 | YOLATHA BAZIL | Anatambulika |
| 300 | ZAKARIA NBII | Anatambulika |
| 301 | ZERNO T. LUKWEMBA | Anatambulika |

## 1.0 KUFUNGULIWA KWA MKUTANO

Mwenyekiti alifungua mkutano saa 03:45 asubuhi.

## 2.0 KUPITISHWA KWA AJENDA

Ajenda zifuatayo zilipitishwa:

1. Kufunguliwa kwa mkutano;
2. Kupitishwa kwa ajenda;
3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili wa Mwaka uliofanyika Julai 31, 2021;
4. Kupokea na kujadili mambo yanayotokana na Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili wa Mwaka uliofanyika tarehe 31 Julai 2021;
5. Kupokea, kujadili na kuidhinisha taarifa ya Wakurugenzi kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2021;
6. Kupokea, kujadili na kuidhinisha taarifa za fedha za Benki na taarifa ya mkaguzi wa nje kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2021;
7. Uteuzi wa wakaguzi wa nje;
8. Kupendekeza tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka ujao;
9. Mengineyo; na
10. Kufungwa kwa Mkutano

## 3.0 UTHIBITISHO WA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KUMI NA MBILI ULIOFANYIKA TAREHE 31 JULAI, 2021.

3.1 Wanahisa walithibitisha kuwa kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili wa Mwaka uliofanyika tarehe 31 Julai, 2021 zilizowasilishwa zilikua sahihi.

## 4.0 KUPOKEA NA KUJADILI MAMBO YATOKAYO KATIKA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KUMI NA MBILI ULIOFANYIKA TAREHE 31 JULAI, 2021.

4.1 IMERIPOTIWA kwamba agizo la wanahisa kwa Bodi ya Wakurugenzi katika kutafuta njia bora ya kuipa mtaji benki lilitekelezwa kwa maana kwamba benki hiyo ilipata mkopo wa chini wa TZS2.7 bilioni Januari 2022.

4.2 IMERIPOTIWA kwamba Benki Kuu ya Tanzania iliwaidhinisha wakurugenzi wapya waliochaguliwa na walianza majukumu yao Januari 27, 2022.

4.3 IMERIPOTIWA kwamba agizo la kufanyika Mkutano Mkuu wa 13 wa Mwaka Julai 30, 2022 lilitekelezwa kwa kuwa mkutano huo ulifanyika katika tarehe iliyopendekezwa.

## 5.0 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA TAARIFA YA WAKURUGENZI KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2021.

5.1 IMERIPOTIWA kwamba benki iliendelea na utoaji wa huduma za kibenki na huduma zinazohusiana kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 2006 ya Mabenki na Taasisi za Kifedha na kwamba hakukuwa na mabadiliko yoyote katika shughuli za msingi za kibenki kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2021.

5.2 IMERIPOTIWA kwamba jumla ya hisa 22,820,059,500 zililipwa mwishoni mwa mwaka 2021.

5.3 IMERIPOTIWA kwamba jumla ya wakurugenzi wanane (8) akiwamo Mkurugenzi Mtendaji walihudumia benki katika kipindi hicho na hakuna Mkurugenzi aliyemiliki zaidi ya asilimia 0.3 ya jumla ya mtaji wa hisa wa Benki uliotolewa.

5.4 IMERIPOTIWA kwamba Bodi ya Wakurugenzi iliendelea kuwajibika katika kuhakikisha kwamba taratibu na kanuni zake zote zinazingatiwa kwa mujibu wa taratibu za uendeshaji wa Benki. Zaidi ya hayo, shughuli za kila siku za mabenki zilikuwa chini ya Mkurugenzi Mtendaji akisaidiwa na Timu ya Menejimenti.

5.5 IMERIPOTIWA kwamba Benki ilipata faida halisi baada ya kodi ya TZS 3 bilioni ikilinganishwa na TZS 3.8 bilioni iliyoripotiwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2020. Vipimo vingine vya utendaji vya benki vilikuwa kama ifuatavyo: -

5.5.1 Benki ilipata jumla ya mapato yote kabla ya tengo la mikopo chechefu la TZS 19.73 bilioni, ikiwa ni ongezeko kidogo ikilinganishwa na TZS 19.50 bilioni zilizoripotiwa mwaka 2020.

5.5.2 Jumla ya mali za benki zilipungua kwa asilimia 1 hadi TZS 216.8 bilioni ikilinganishwa na TZS 219.9 bilioni zilizoripotiwa mwaka 2020.

5.5.3 Mikopo halisi ilishuka kwa asilimia 5 hadi TZS 115.0 bilioni ikilinganishwa na TZS 123.4 bilioni zilizoripotiwa kwa mwaka uliotangulia. Hata hivyo, ubora wa kitabu cha mikopo uliimarika kidogo kwa kufikia uwiano wa mikopo Chechefu wa asilimia 9 ikilinganishwa na asilimia 10 iliyoripotiwa mwaka 2020.

5.5.4 Jumla ya gharama za uendeshaji zilipungua kwa asilimia 3 hadi TZS 15.56 bilioni kutoka TZS 16.0 bilioni. Hii ilichangiwa na kuendelea kwa benki kuzingatia mipango ya usimamizi wa gharama.

5.5.5 Amana za wateja zilifikia TZS 181.5 bilioni, ikiwa ni pungufu kwa asilimia 1.3 kutoka TZS 183.9 bilioni zilizoripotiwa mwaka uliotangulia.

5.5.6 Fedha za wanahisa ziliongezeka kwa asilimia 26 hadi TZS 25.82 bilioni kutoka TZS 20.57 bilioni zilizoripotiwa mwaka uliotangulia.

5.6 IMERIPOTIWA kwamba Bodi ya Wakurugenzi ilifanya tathmini kuhusu uwezo wa Benki kuendelea kufanya biashara na matokeo yalionyesha kwamba Benki itaweza kufanya shughuli zake kwa muda mrefu bila shida.

5.7 IMERIPOTIWA kwamba Bodi ya Wakurugenzi haikupendekeza malipo ya gawio kwa wanahisa kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2021 kutokana na ukweli kwamba Benki haikukidhi vigezo vya Uwiano wa Gharama za Uendeshaji na Mapato Ghafi wa asilimia 55 vilivyoainishwa na Benki Kuu ya Tanzania ili kupata malipo ya gawio na kwamba Benki ilikuwa katika mchakato wa kuongeza mtaji wa biashara yake.

5.8 IMERIPOTIWA kwamba Benki ilikuwa na wafanyakazi wa kutosha na wenye uzoefu wa kutekeleza shughuli zao na kutimiza mpango wa biashara wa Benki.

5.9 IMERIPOTIWA kwamba Benki haikutoa msaada kwa vyama vya siasa na iliendelea kuwa na uhusiano mzuri na wadau wote zikiwamo taasisi za usimamizi wa mabenki.

5.10 IMERIPOTIWA kwamba benki ilifanikiwa kukamilisha na kuzindua miradi ya kidijitali inayojumuisha Huduma za Kibenki kupitia Mawakala (Mkombozi WAKALA), Huduma za Kibenki za Intaneti, Huduma za Usimamizi wa Fedha na Huduma za Programu za App za Simu Janja.

5.11 IMERIPOTIWA kwamba benki iliendelea na kuongeza mtaji kupitia urekebishaji wa mikopo ambayo malipo yake hayakwenda sawa na matarajio ya urejeshaji faida ili itumike kutunisha mtaji na kukusanya mtaji kwa kuwaruhusu wanahisa kununua hisa zaidi.

5.12 IMERIPOTIWA kwamba benki iliendelea kutekeleza mfumo madhubuti wa ukopeshaji ambao ulikuwa unashughulikia majukumu muhimu ya mikopo, ambayo ni utoaji wa mikopo bora, usimamizi wa malipo ya mikopo kwa wakati na urekebishaji wa mikopo inayodorora ili kuwa na usimamizi mzuri wa mikopo na ulipaji wake.

5.13 IMERIPOTIWA kwamba wanahisa walibaini yafuatayo kutokana na majadiliano hayo:

5.13.1 Benki ilionekana kutoendana na dira yake ya awali ya kushughulika na biashara ndogo ndogo na badala yake lengo lake kuu lilikuwa kwenye mikopo ya kibiashara. Benki iliripoti kwamba mkazo uliwekwa kwenye mikopo midogo midogo kupitia Mikopo ya Kundi la Mshikamano (SGL) na mikopo ya watumiaji;

5.13.2 Benki ilishindwa kuendeleza dhamira ya kutoa gawio kwa wanahisa. Benki iliripoti kwamba hii ilichangiwa na matarajio ya ukuaji wa benki ambayo yanahitaji rasilimali zaidi za kifedha na vilevile ukomo wa Uwiano wa Gharama za Uendeshaji na Mapato Ghafi wa asilimia 55 kama sharti la malipo ya gawio;

5.13.3 Benki ilitoa mikopo kwa taasisi zinazohusiana na Kanisa ambazo hazikuweza kuhudumia mikopo yao kwa kiasi cha kutishia uhai wa benki. Benki iliripoti kwamba hakuna taasisi za Kanisa ambazo mikopo yake haikulipwa kwa wakati na kwamba Changamoto za kihistoria za mikopo isiyolipika zilirekebishwa na zinaendelea kurekebishwa bila kujali aina ya taasisi au mkopaji.

5.13.4 Benki haikuchukua hatua muhimu dhidi ya wafanyakazi wake waliohusika katika utoaji wa mikopo mibaya ambayo iliiweka hatarini Benki. Benki iliripoti kwamba masuala ya wafanyakazi kuhusika katika utoaji wa mikopo mibovu kwa kawaida hushughulikiwa ipasavyo na hatua zinazofaa huchukuliwa dhidi ya wale ambao wamethibitika kutokuwa waaminifu au wazembe katika utoaji wa mikopo hiyo.

5.13.5 Benki haikuweka orodha ya mikopo iliyotolewa kwa wafanyakazi wake kwa kuwa hii haikuwa ajenda rasmi ya Mkutano Mkuu wa Mwaka.

5.13.6 Kwamba taaarifa na nyaraka muhimu kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa Mwaka hazikuwafikia baadhi ya wanahisa kwa wakati.

5.13.7 Kwamba Mikopo Isiyolipika ilikuwa tishio kwa biashara ya benki kutokana na mambo mbalimbali ikiwamo ukosefu wa elimu na mafunzo kwa baadhi ya maofisa mikopo.

6.0 IMERIPOTIWA kwamba wanahisa walitoa MAELEKEZO yafuatayo kulingana na mjadala hapo juu: -

6.1 Kuimarisha kitengo cha mikopo midogo midogo ya biashara ya benki ili kufufua dira ya kushughulika na biashara ndogondogo.

6.2 Benki itoe taarifa ya idadi ya mikopo na salio la mikopo iliyotolewa kwa wafanyakazi wake wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka.

6.3 Benki ihakikishe kwamba matangazo na nyaraka muhimu kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa Mwaka zinasambazwa kwa Wanahisa kwa wakati.

6.4 Benki iongeze utoaji mafunzo kwa wafanyakazi wake ili waelewa mbinu mbalimbali za jinsi ya kusimamia mikopo mizuri kuanzia mwanzo.

7.0 Wanahisa wa Benki walipokea, walijadili na kuidhinisha ripoti ya Bodi ya Wakurugenzi.

## 8.0 KUPOKEA, KUJADILI NA KUIDHINISHA TAARIFA ZA FEDHA ZA BENKI NA TAARIFA YA MKAGUZI WA NJE KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2021.

8.1 IMERIPOTIWA kwamba wakaguzi wa nje wa Benki kwa mwaka 2021 walikuwa Ernst & Young.

8.2 IMERIPOTIWA kwamba kufikia Desemba31, 2021, Wakaguzi walifanya marejeo ya mizania ya Benki, mapato, taarifa ya mabadiliko katika suala la hisa zisizo na riba, taarifa ya mtiririko wa fedha ya kila mwaka, muhtasari wa sera na maelekezo mengine ya kifedha kutoka mwaka uliotangulia.

8.3 IMERIPOTIWA kwamba katika maoni ya Wakaguzi wa Hesabu, taarifa za fedha zilizokaguliwa zilionyesha Benki kuwa katika nafasi nzuri kifedha kufikia Desemba 31, 2021, kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Taarifa za Fedha (IFRS) na matakwa ya Sheria ya Kampuni mwaka 2002 na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006.

8.4 IMERIPOTIWA kwamba Wakaguzi walifanya ukaguzi kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (IAS).

8.5 IMERIPOTIWA kwamba Wakaguzi walipata taarifa na maelezo yote ambayo kwa ufahamu na imani yao zilikuwa muhimu kwa ajili ya ukaguzi wao.

8.6 IMERIPOTIWA kwamba katika maoni ya Wakaguzi, vitabu sahihi vya hesabu vilitunzwa na Benki na kwamba Ripoti ya Wakurugenzi iliendana na taarifa za fedha. Taarifa zilizoainishwa na sheria kuhusu malipo ya Wakurugenzi na miamala na Benki ziliwekwa wazi na taarifa ya hali ya fedha ya Benki na taarifa ya faida au hasara na mapato mengine ya kina yaliendana sawa na vitabu vya hesabu.

8.7 IMERIPOTIWA kwamba katika maoni ya wakaguzi, uwiano wa utoshelevu wa mtaji wa benki uliowasilishwa ulifanyiwa mahesabu kwa mujibu wa Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya waka 2006 na Kanuni za Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha (Utoshelevu wa Mtaji) ya mwaka 2014 na matamko yanayohusiana na Benki Kuu ya Tanzania.

8.8 Wanahisa walipokea, walijadili na kuridhia /kupitisha taarifa za fedha za Benki na ripoti ya mkaguzi wa nje kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2021 kama ilivyowasilishwa.

## 9.0 UTEUZI WA MKAGUZI WA NJE

9.1 IMERIPOTI kwamba mkataba na Ernst & Young (EY) kama wakaguzi wa nje wa benki uliisha Desemba 2021.

9.2 IMERIPOTIWA kwamba kufuatia kumalizika kwa mkataba na hatimaye kuondoka kwa kampuni ya Ernst & Young (EY), benki ilipendekeza wakaguzi wengine wa nje kuchukua jukumu hilo.

9.3 IMERIPOTIWA kwamba Benki ilipendekeza KPMG, PWC Tanzania, Claritas, HLB na Innovex kama wakaguzi wanaofaa kuwa wakaguzi wa nje wa benki kwa miaka mitatu ijayo kuanzia 2022. Benki iliripoti pia ada za kitaaluma zilizopendekezwa na kila kampuni tajwa hapo juu kama ujira wa ukaguzi wa hesabu katika kipindi hicho.

9.4 IMERIPOTIWA kwamba kutokana na uzoefu na uwezo mkubwa wa kitaaluma, Bodi ya Wakurugenzi ilipendekeza PWC Tanzania kuwa wakaguzi wa nje wa hesabu za benki kwa miaka mitatu ijayo.

9.5 Wanahisa walijadili na kuridhia/kupitisha kuwateua PWC Tanzania kama Wakaguzi wa Benki wa nje kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2022 hadi mwaka 2024.

## 10.0 KUPANGA TAREHE YA MKUTANO MKUU WA MWAKA UJAO

10.1 IMERIPOTIWA kwamba wanahisa waliamua kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka unaofuata ufanyike tarehe 29 Julai, 2023.

## 11.0 MENGINEYO

11.1 IMERIPOTIWA kwamba wanahisia walisisitiza Bodi kuhakikisha kwamba ujumbe wa mwaliko wa Mikutano mikuu ya miaka ijao inasambazwa mapema kwa wanahisa wote.

11.2 IMERIPOTIWA kwamba benki ilitakiwa kushirikisha na kuendelea kufanya kazi kwa ukaribu na Kanisa Katoliki na Taasisi zake mbali mbali ili kunufaika na idadi kubwa ya wateja wanaopatikana ndani ya mtandao wa Kanisa.

## 12.0 KUFUNGWA KWA MKUTANO

12.1 Mwenyekiti alifunga mkutano saa 9:26 mchana.

Imethibitishwa leo tarehe 29 Julai, 2023.

| | |
|---|---|
| Bw. Gasper Njuu | Bi. Paulina Kunjumu |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

AJENDA YA 4

# YATOKANAYO NA MKUTANO WA 13 WA MWAKA ULIOFANYIKA JULAI 30, 2022

| KUMB. NO. | MAAZIMIO YA WANAHISA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 6.1 | Kuimarisha kitengo cha mikopo ya wajasiriamali wadogo na kuupa kipaumbele mtazamo wa taasisi kushughulikia masuala ya biashara ndogondogo | Benki imefanikiwa kukuza kitengo cha mikopo ya wajasiriamali wadogo kupitia mikopo ya vikundi na thamani ya mikopo imeongezeka kwa TZS bilioni 2.10 kutoka TZS bilioni 3.64 2021 hadi TZS bilioni 5.73 mwaka 2022. Benki inaendelea kuipa kipaumbele sekta ya biashara ndogondogo kwa kutangaza mikopo ya vikundi kwenye mtandao wake na matawi kote nchini. |
| 6.2 | Kutoa taarifa za idadi ya mikopo na kiasi cha madeni kilichotolewa kwa wafanyakazi wa benki kwenye mkutano wa mwaka. | Kwa mwisho wa mwaka 2022 Benki ilikuwa na jumla ya mikopo 150 yenye thamani ya TZS 1,098,055,316.47 kwa wafanyakazi wake.<br><br>Marejesho ya mikopo hiyo yanaendelea vizuri kwa mujibu wa taratibu na makubaliano ya mikopo hiyo. |
| 6.3 | Benki ihakikishe taarifa na vifaa muhimu vitakavyotumika kwenye mkutano mkuu vinawafikia wanahisa kwa wakati. | Bodi ya wakurugenzi ilihakikisha taarifa na vifaa muhimu vya mkutano wa 14 wa mwaka vimefikishwa kwa wanahisa kwa wakati muafaka. |
| 6.4 | Benki kuimarisha mafunzo kwa wafanyakazi ili kuwaongezea ujuzi wa utoaji na usimamiaji mzuri wa mikopo inayotolewa na benki kwa wateja wake | Mafunzo ya jinsi ya kufanya uchambuzi na kusimamia mikopo ni mpango endelevu kwa benki. Kila mwaka Benki inaandaa mafunzo maalumu yanayojikita kwenye eneo hili. |

## AJENDA YA 5

### 5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA TAARIFA YA WAKURUGENZI YA MWAKA ULIOISHIA DESEMBA 31, 2022.

### 5.1 KAZI KUU

Kazi kuu ya benki hii ni utoaji wa huduma za kibenki na huduma zinazohusiana na hizo kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006. Hakukuwa na mabadiliko kwenye shughuli za kibenki katika mwaka huu wa fedha.

### 5.2 MTAJI WA BENKI

Mtaji wa Benki hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2022 ni kama ilivyoonyeshwa hapa chini: -

| Mtaji Uliohidhinishwa |
|---|
| TZS 50,000,000,000 inayojumuisha hisa 50,000,000 za kawaida zenye thamani ya TZS 1,000 kila hisa mmoja. |

**Hiza zilizolipwa:**

TZS 22,820,069,500 inayojumuisha hisa za kawaida 23,555,002, kila hisa ikiwa na thamani ya TZS 1,000/=. Sehemu ya hisa hizi iliuzwa kwa bei pungufu kama inavyoahinishwa kwenye kumbukumbu namba 35 ya taarifa za fedha.

### 5.3 MGAWANYO WA WANAHISA WA BENKI

Hadi kufikia Desemba 31, 2022, umiliki wa hisa ulikuwa kama ifuatavyo:

| WAMILIKI | IDADI YA HISA | THAMANI | % YA UMILIKI |
|---|---:|---:|---:|
| Majimbo ya Kanisa Katoliki na taasisi zake | 7,049,049 | 6,731,213,750 | 29.50% |
| Taasisi nyingine | 2,235,141 | 2,207,832,500 | 9.67% |
| Baraza la Maaskofu | 4,133,995 | 4,133,995,000 | 18.12% |
| Watu binafsi | 10,136,817 | 9,747,028,250 | 42.71% |
| **Jumla** | 23,555,002 | 22,820,069,500 | 100.0% |

Hadi kufikia tarehe Desemba 31, 2021 umiliki wa hisa ulikuwa kama ifuatavyo:

| AINA | IDADI YA HISA | THAMANI | % YA UMILIKI |
|---|---|---|---|
| Majimbo ya Kanisa la Katoliki na taasisi zake | 7,049,049 | 6,731,213,750 | 29.50% |
| Taasisi nyingine | 2,235,141 | 2,207,832,500 | 9.67% |
| Baraza la Maaskofu | 4,133,995 | 4,133,995,000 | 18.12% |
| Watu binafsi | 10,136,817 | 9,747,028,250 | 42.71% |
| JUMLA | 23,555,002 | 22,820,069,500 | 100.0% |

## 5.4 WAKURUGENZI

Wakurugenzi wa Benki ambao waliotumikia Benki kwa kipindi chote cha mwaka 2022 ni kama ifuatavyo: -

| JINA | WADHIFA | UMRI | TAALUMA/SIFA | TAIFA | TAREHE YA UTEUZI/ KUJIU ZULU |
|---|---|---|---|---|---|
| Bw. Gasper Njuu | Mwenyekiti | 63 | Diploma ya Juu ya Benki, Stashahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Fedha, Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara (MBA) Kimataifa | Tanzania | Januari 27, 2022 |
| Bw. Respige O. Kimati | Mkurugenzi Mtendaji | 48 | Shahada ya Biashara katika Fedha, Shahada ya Uzamili (MSc) katika Fedha | Tanzania | Januari 18, 2020 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya | Mjumbe | 65 | Askofu Mkuu Dayosisi ya Dodoma,<br><br>Shahada ya Uzamili katika Historia, Shahada ya Jiografia, Shahada ya Theolojia | Tanzania | Aliteuliwa tena Mei 30, 2015 |
| Bw. Martin Mdoe | Mjumbe | 51 | Wakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Shahada ya Sheria (LLB), Shahada ya Juu ya Sheria (LLM) na Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara (MBA). | Tanzania | 27 Januari 2022 |
| Bw. Robert Mtendamema | Mjumbe | 49 | Shahada ya Sayansi ya Kompyuta na Shahada ya Uzamili ya Sayansi Mifumo ya Mawasiliano ya Data. | Tanzania | 8 Agasti 2018 |
| Bi. Uphoo Swai | Mjumbe | 50 | Mhasibu wa Umma Aliyeidhinishwa (CPA), Diploma ya Juu ya Uhasibu, Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara. | Tanzania | 8 Agasti 2018 |
| Bw. Benedict Warisianga Sudi | Mjumbe | 54 | Mhasibu wa Umma Aliyeidhinishwa (CPA), Diploma ya Juu ya Uhasibu. | Tanzania | 9 Mei 2019 |
| Padri. Dk. Charles Kitima | Mjumbe | 57 | Shahada ya Sanaa katika Theolojia, Leseni katika Sheria za Canon na Shahada ya Uzamivu ya Sheria. | Tanzanian | 2 Januari 2019 |

Wakurugenzi wafuatao wanamiliki hisa hadi kufikia mwaka huu:

| Jina la Mkurugenzi | Idadi ya hisa | |
|---|---|---|
| | **2022** | **2021** |
| Mhasham Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya | 13,574 | 13,574 |
| Prof. Marcellina Mvula Chijoriga* | 17,000 | 17,000 |
| Bw. Ayoub Mtafya* | 6,250 | 6,250 |
| Bw. Robert Mtendamema | 1,190 | 1,190 |
| Bw. Respige Onesmo Kimati | 260 | - |
| **Jumla ya hisa zinazomilikiwa na wakurugenzi** | **38,274** | **38,014** |

Hakuna mkurugenzi aliyemiliki zaidi ya asilimia 0.1 ya hisa zilizotolewa na Benki.

*Ujumbe wa Prof. Marcelina Chijoriga's na Bw. Ayoub Mtafya kwenye bodi ulikoma mnamo Januari 26, 2022.

## 5.5 KATIBU KAMPUNI

Hadi kufikia Mei 2022 Katibu wa Benki alikuwa ni Bwana Baltazar Mbilinyi ambaye mkataba wake ulimalizika Mei 2022.

## 5.6 UONGOZI WA KAMPUNI

Bodi ya Wakurugenzi inajumuisha wajumbe wanane akiwamo Mkurugenzi Mtendaji. Hakuna Mkurugenzi anayeshikilia wadhifa wa kiutendaji ndani ya benki isipokuwa Mkurugenzi Mtendaji tu. Bodi ya Wakurugenzi inawajibu wa kuainisha maeneo ambayo ni nyeti kiutendaji, kuzingatia na kufuatilia maamuzi ya uwekezaji, kuzingatia masuala muhimu ya kifedha na kufanya tahmini ya utendaji ya menejimenti juu ya mipango ya biashara na bajeti.

Pia, bodi ina wajibu wa kuhakikisha kuna mfumo wa ndani unafanya kazi kwa usahihi kudhibiti sera na taratibu ambao unaendana na taratibu za kiutawala.

Bodi ya Wakurugenzi inatakiwa kukutana angalau mara nne kwa mwaka. Wajumbe wa bodi watakabidhi shughuli za kila siku za uongozi kwa Mkurugenzi Mtendaji ambaye atasaidiana na timu yake ya uongozi. Timu ya uongozi itakaribishwa kuhudhuria vikao vya Bodi ya Wakurugenzi na pia inawajibu wa kuwa mhimili wa mawasiliano na idara mbalimbali za benki ili kuwezesha shughuli za kila siku za uendeshaji wa benki.

**Mahudurio ya Wakurugenzi yalikua kama ifuatavyo: -**

| No. | Jina la mjumbe | Cheo | Idadi ya mikutano | Mikutano aliyohudhuria | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Gasper Njuu | Mwenyekiti wa bodi | 9 | 9 | 100% |
| 2. | Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya | Mjumbe | 9 | 9 | 100 % |
| 3. | Bw. Benedict Sudi Warisianga | Mjumbe | 9 | 9 | 100% |
| 4. | Bw. Martin Mdoe | Mjumbe | 9 | 9 | 100% |
| 5. | Bi. Uphoo Swai | Mjumbe | 9 | 9 | 100% |
| 6. | Padri. Dk. Charles Kitima | Mjumbe | 9 | 9 | 100% |
| 7. | Bw. Robert Mtendamema | Mjumbe | 9 | 8 | 89% |
| 8. | Prof. Marcellina Chijoriga * | Mjumbe | 9 | 1 | 11% |
| 9. | Bw. Ayoub Mtafya* | Mjumbe | 9 | 1 | 11% |

*Ujumbe wa Prof. Marcelina Chijoriga's na Bw. Ayoub Mtafya kwenye bodi ulikoma mnamo Januari 26, 2022.

Bodi ina kamati tatu ambazo ni kamati ya ukaguzi, ukubalifu na vihatarishi, kamati ya rasilimali watu na uendeshaji wa benki na kamati ya mikopo. Kila kamati ina mwongozo katika kutekeleza wajibu wake ili kuhakikisha ufanisi na matokeo kwenye utekelelaji wa majukumu ya bodi.

Benki imejikita kwenye taratibu na matokeo chanya ya kiutendaji hususani kwa kutambua umuhimu wa uadilifu, uwazi na uwajibikaji. Bodi inaangalia kwa karibu shughuli za benki ili kuhakikisha kuwapo kwa viwango vya juu vya uongozi wa taasisi kupitia kamati zake kama inavyoainishwa hapa chini:

### Kamati ya ukaguzi, ukubalifu na vihatarishi inaundwa wafuatao:

| No. | Jina la mkurugenzi | cheo | Idadi ya mikutano | Mikutano aliyohudhuria | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bi. Uphoo Swai | Mwenyekiti | 8 | 8 | 100% |
| 2. | Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya | Mjumbe | 8 | 8 | 100% |
| 3. | Bw. Benedict Warisianga Sudi | Mjumbe | 8 | 8 | 100% |

### Kamati ya mikopo inaundwa na wafuatao:

| No. | Jina la mkurugenzi | Cheo | Idadi ya mikutano | Mikutano aliyohudhuria | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Robert Mtendamema | Mwenyekiti | 8 | 8 | 100% |
| 2. | Bw. Martin Mdoe | Mjumbe | 8 | 7 | 88% |
| 3. | Padri. Charles Kitima | Mjumbe | 8 | 7 | 88% |
| 4 | Bw. Ayoub Mtafya | Mjumbe | 8 | 1 | 13% |

### Kamati ya rasilimali watu na uendeshaji wa benki inaundwa na wafuatao:

| No. | Jinalamkurugenzi | Cheo | Idadi ya mikutano | Mikutano aliyohudhuria | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Martin Mdoe | Mwenyekiti | 5 | 4 | 80% |
| 2. | Bw. Robert Mtendamema | Mjumbe | 5 | 5 | 100% |
| 3. | Padri Charles Kitima | Mjumbe | 5 | 4 | 80% |
| 4 | Bw. Ayoub Mtafya | Mjumbe | 5 | 1 | 20% |

## 5.7 MENEJIMENTI

Mkurugenzi Mtendaji alisaidiwa na wakuu wa idara kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| • Afisa Mkuu wa Fedha<br>• Afisa Mkuu wa Undeshaji wa Benki<br>• Mkuu wa Idara ya Hazina<br>• Mkuu wa Idara ya Mikopo<br>• Afisa Mkuu wa Ukaguzi wa Ndani<br>• Afisa Mkuu wa Biashara | • Mkuu wa idara ya mifumo na tehama<br>• Mkuu wa idara ya huduma za sheria (Katibu wa Kampuni)<br>• Meneja wa Ukubalifu na Vihatarishi<br>• Meneja wa Rasilimali watu na Ajira. |

Taarifa zaidi za utendaji zimo kwenye aya ya 5.8 kwenye taarifa ya Wakurugenzi.

## 5.8 UWEZO WA KIFEDHA NA HALI ILIVYO

Benki iliripoti kupata faida kabla ya kodi ya kiasi cha TZS 5,145 milioni katika mwaka ulioishia Desemba 31, 2022 (taarifa ya mwaka 2021 iliripoti hasara ya TZS 2,707 milioni kabla ya kodi): -

- Mapato halisi ya kiuendeshaji yalikuwa TZS 21,096 milioni ikilinganishwa na TZS 12,954 milioni za mwaka 2021 ikionyesha kushuka kwa gharama za riba TZS 1,298 milioni ambayo ni asilimia 16 zilizochangiwa na uhamasishaji wa amana nafuu, ongezeko la mapato ya riba kwa TZS 3,6 bilioni zilizochangiwa na ongezeko la mikopo na mikopo ya awali na rekebisho la faida la TZS 1.02 bilioni (mwaka 2021 rekebisho la faida lilikuwa TZS 2.7 bilioni).
- Amana za wateja ziliongezeka kwa TZS 184,578million ikilinganishwa na TZS 184,578 milioni za mwaka 2021. Ongezeko hili lilichangiwa na juhudi za uhamasishaji zilizofanyika.
- Thamani ya mali za benki ziliongezeka kwa TZS 221,722 millioni ikilinganishwa na TZS 210,379 million mwaka 2021 kuliko changiwa na ongezeko la mikopo kwa wateja na benki nyingine.
- Gharama za uendeshaji zilikuwa TZS 15,951 milioni ikilinganishwa na TZS 15,661 milioni mwaka 2021 ikiwa ni ongezeko dogo la asilimia 2 na kuashiria ongezeko la shughuli za kibiashara.

- Mikopo iliongezeka kwa TZS 115,039 millioni ikilinganishwa na mwaka 2021 ambapo mikopo iliyotolewa ilikuwa na thamani ya TZS 106,860 millioni ikiwa ni ongezeko la asilimia 9.

**Viashiria muhimu vya utendaji benki ni kama ifuatavyo:**

| Kiashiria cha Utendaji | Tafsiri na njia ya kufanya hesabu | 2022 | 2021 Imerekebishwa |
|---|---|---|---|
| Uwiano wa Mapato na Hisa | Faida au(Hasara) Kabla ya Kodi auJumla ya Hisa | 20% | (15%) |
| Uwiano wa Mapato na Mali | Faida au(Hasara) Kabla ya Kodi auJumla ya Mali | 2% | (1%) |
| Uwiano wa Gharama na Mapato | Gharama za Uendeshaji/Mapato halisi ya Riba na Yasiyo ya Riba | 62% | 90% |
| Uwiano wa Riba na Mali izalishayo | Mapato yoye ya Riba/ (Riba inayopatikana kutokana na amana za serikali + Salio katika benki nyingine + Mikopo iliyopokelewa kutoka benki nyingine + Uwekezaji katika Amani nyinginezo + Mikopo) | 12% | 13% |
| Uwiano wa Mapato yasiyo ya riba na Mapato Ghafi | Mapato Yasiyo ya Riba/Mapato Yote | 18% | 23% |
| Uwiano Mapato kwa kila Hisa | Mapato ya Msingi/Idadi ya Hisa za kawaida kwa Shilingi za Tanzania | 239 | (79) |
| Uwiano wa Mikopo yote na Amana za wateja | Jumla ya Mikopo kwa Wateja/ Jumla ya Amana za Wateja | 63% | 59% |
| Uwiano wa Mikopo Chechefu na Mikopo Yote | Mikopo Chechefu/Jumla ya Mikopo Ghafi | 9% | 9% |
| Mali inayoingiza Mapato na Jumla ya Mali | Mali iingizayo Mapato/Mali zote | 84% | 84% |
| Ongezeko la Mali Zote | Mwenendo (Jumla ya Mali 2022 – Jumla ya Mali 2021) | 5% | (3%) |

**Mtaji**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Uwiano wa Mtaji Mkuu (Kundi la Kwanza) | [Mtaji Mkuu/ Jumla ya Kiwango vihatarishi tarajiwa katika Hali ya Kifedha ya Benki, Kiwango cha ukosefu wa kinga kwa Benki juu ya Vihatarishi vya kiutendaji na vya sokoni x 100 | 13.05% | 9% |
| Uwiano wa Mtaji wa Jumla (Kundi la Kwanza + Kundi la Pili) | [Jumla ya Mtaji/Jumla Kiwango cha Vihatarishi Total Capital/ Total Risk-weighted on and off statement of financial position, operational and market risk weighted exposures] x 100 | 14.84% | 9% |

Benki lilipata faida kabla ya kodi ya TZS 5,145 milioni kwenye mwaka ulioishia Desemba 31, 2022 ikilinganishwa na TZS 2,706 milioni mwaka 2021. Mtaji uliowekezwa na uwiano wa jumla wa mtaji ulikuwa TZS 9,621 milioni na TZS 22,321 milloni, TZS 19,621 milioni na TZS 22,321 milioni, ni 13.05% na 14.84% kwa pamoja (2021: TZS 12,190 milioni, 9% na 9%). Wakurugenzi wanathibitisha kuwa viwango vilivyotumika vimefuata taratibu na kwamba taarifa za fedha zimetayarishwa kwa umakini.

## 5.9 MATAWI NA MITANDAO YA BENKI

Benki ina matawi kumi na moja hadi kufikia Desemba 31 2022; manne yakiwa Dar es Salaam na tawi moja moja kwenye mikoa ya Mwanza, Kagera, Morogoro, Dodoma, Iringa Njombe na Kilimanjaro.

Jumla ya wakopaji na wenye akaunti hadi kufikia mwishoni mwa mwaka ni kama ifuatavyo:

| | 2022 | 2021 |
|---|---|---|
| **Aina ya Akaunti** | | |
| Akaunti za Hundi | 4,177 | 3,615 |
| Akaunti za Amana | 88,804 | 72,417 |
| Akiba za Muda Maalumu | 727 | 878 |
| **Idadi ya akaunti za akiba** | **93,708** | **76,910** |
| **Akaunti za mikopo** | **13,991** | **10,883** |

## 5.10 GAWIO

Wakurugenzi wa Bodi hawapendekezi kutolewa kwa gawio kwa mwaka ulioshia tarehe 31 Desemba, 2022.

## 5.11 MAENDELEO MUHIMU KATIKA MWAKA

- Kujitoa kwa benki na kuzingatia ushirikishwaji kwenye sekta ya fedha kunabakia kuwa kipaumbele kikuu cha kimkakati na kwa maana hiyo, benki ilikamilisha ushirikiano na wadau na washirika mbalimbali katika utoaji wa huduma za kifedha kidijitali hasa kwa kushirikiana na mitandao ya simu na viunganishi vingine vya kutatua changamoto za kijiditali.

- Benki ilipata mafanikio kwa kuzindua mtandao wa wakala ujulikanao kama Mkobozi Wakala, ukusanyaji sadaka kidijitali (SADAKA DIGITAL) na huduma za kibenki kwa njia ya mtandao. Pia benki iliboresha programu ya kibenki kwa njia ya simu ya mkononi kwa kutumia mfumo uliopo wa USSD.

- Benki ilikamilisha mpango wake wa kufungua matawi mapya kwenye miji ya Arusha na Mwanza. Matawi haya yataanza kutoa huduma kabla ya mwisho wa robo ya tatu ya mwaka 2023. Tawi la Arusha limeshafunguliwa mwezi Mei, 2023.

- Benki inakamilisha mpango wa kuhamisha ofisi za makao makuu pamoja na Tawi la Mt. Yosefu kwenda katika Jengo jipya la Mtakatifu Joseph ambalo ni eneo la kimkakati ili kuboresha taswira na kutoa huduma nzuri za kibenki. Uhamisho huu unatarajiwa kukamilika kwenye robo ya tatu ya mwaka 2023.

- Tuliongezea nguvu kikosi chetu cha rasilimali watu kwa kuajiri maofisa wakuu kwenye vitengo muhimu vya fedha na biashara. Tuliimarisha timu yetu ya usimamizi wa mauzo, mahusiano na huduma kwenye mtandao ambayo ni muhimu kwenye kusaidia azma yetu ya ukuaji na kutarajia ubora wa huduma.

- Kwa ujumla, juhudi zetu za kuimarisha biashara na matarajio ya ukuaji zinaendelea kuzaa matunda kama ilivyotafsiriwa kutokana na ongezeko la wateja, viwango vya mapato vilivyoimarika, usimamizi bora wa gharama na uboreshwaji wa huduma muhimu.

### 5.12 MIAMALA NA WANAOHUSIANA NA BENKI

Miamala na wanaohusiana na benki vimewekwa katika kiambatisho namba 38 cha taarifa za fedha

### 5.13 MPANGO WA MAENDELEO

Benki inaendelea kujikita kwenye mpango mkakati wa kufikia lengo la kupata faida zaidi na ukuaji wa benki kwa ujumla. Benki ina mipango ifuatayo: -

- Kuboresha biashara kisasa zaidi kupitia kuanzisha wakala wa benki, huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi, huduma za kibenki za mtandao, tovuti na suluhuhisho katika usimamizi wa fedha na mitandao ya kidijitali;
- Kupanua uwezo wa benki kuwafikia wateja kupitia mawakala wa benki, matawi madogo madogo na vituo vya huduma za fedha;
- Kujikita kwenye soko maalumu ili kusukuma mbele maendeleo ya benki kwa kutilia mkazo azma ya benki ya kuboresha akaunti hususani akaunti za hundi na akaunti za akiba kufikia kiwango cha asilimia 70 na kwa akaunti za akiba za muda maalumu kuwa na asilimia 30 katika kipindi cha mwaka mmoja mpaka mitatu.
- Kuboresha mfumo wa utoaji wa mikopo ili kuleta ufanisi na faida kwa benki ndani ya muda wa kati ya mwaka mmoja hadi miaka mitatu;
- Kuongeza juhudi katika kupunguza gharama za uendeshaji lengo likiwa ni kupata uwiano wa matumizi na mapato wa asilimia 55 kwa kipindi cha kati ya mwaka mmoja na miaka mitatu;
- Kuhamasisha wafanyakazi kwa kuwaongezea ujuzi katika kusimamia mfumo na utendaji;
- Kuimarisha mfumo wa usimamizi wa huduma kwa wateja ili kuboresha utoaji huduma na uzoefu kwa wateja;
- Kuimarisha ubunifu na uwekezaji kwenye teknolojia ili kutoa huduma zenye viwango bora na kuboresha umahiri kwenye huduma kwa wateja.

### 5.14 RASILIMALI WATU

Benki ina wafanyakazi wa kutosha wenye uwezo na uzoefu wa kutosha katika nafasi zote muhimu.

### 5.15 VIHATARISHI

Kadiri Benki inavyoendelea kukuza uendeshaji wake inahakikisha kwamba hali hatarishi inadhibitiwa kwa mujibu wa sera na taratibu zote zilizowekwa. Shughuli za kibenki zinazoweza kuwekwa katika hali hatarishi zinajumuisha shughuli za mikopo, hali ya ukwasi, athari za masoko na athari za kisera. Masuala yote yahusuyo usimamizi wa hali hatarishi yameainishwa na Bodi ya Wakurugenzi kwenye sera za Benki ambazo zinatekelezwa na Menejimenti ya Benki.

### 5.16 USIMAMIZI WA HALI HATARISHI NA UDHIBITI WA NDANI

Bodi ya Wakurugenzi inazingatia uwajibikaji wake wa mwisho wa kusimamia hali hatarishi na kuhakikisha panakuwepo mfumo wa udhibiti wa ndani kwa ajili ya utendaji bora na kuhifadhi mali za Benki. Ni jukumu la Bodi kuhakikisha kuwa mifumo thabiti na endelevu ya udhibiti wa fedha na utendaji inatengenezwa, kuhakikiwa na kubadilishwa kila inapobidi ili kuhakikisha yafuatayo yanatekelezwa: -

- Uendeshaji kwa ufanisi na tija wa shughuli za kibenki;
- Kulinda mali za Benki;
- Kuzingatia sheria husika na taratibu za uendeshaji wa Benki;
- Kuhakikisha usahihi wa vitabu vya hesabu na kumbukumbu za miamala ya fedha za Benki;
- Kuhakikisha uendelevu wa shughuli za Benki katika mazingira ama ya kawaida au hatarishi; na
- Kuwa na tabia ya uwajibikaji kwa wadau wote wa Benki.

Ufanisi wa mfumo wa udhibiti wa ndani unategemea utekelezaji halisi wa taratibu na kanuni zilizowekwa. Mara nyingi kunakuwepo na uwezekano wa wafanyakazi kutozingatia taratibu zilizowekwa. Hakuna mfumo wa udhibiti wa ndani unaoweza kuweka kinga

kamilifu dhidi ya makosa ya uhasibu au vitendo vya kusababisha hasara. Hata hivyo mfumo wa Benki uliopo umetengenezwa ili kuihakikishia Bodi kwa kiwango cha kuridhisha kuwa taratibu zilizopo zinazingatiwa kwa ufanisi.

## 5.17 MAMBO HATARISHI

Kwa maoni ya Wakurugenzi hapakuwepo na hali au kesi zozote zilizopo mahakamani ambazo zingeathiri utendaji wa Benki.

## 5.18 USTAWI WA WAFANYAKAZI

### Uhusiano baina ya menejimenti na wafanyakazi

Uhusiano kati ya wafanyakazi na menejimenti uliendelea kuwa mzuri. Malalamiko yote yanasuluhishwa kutokana na mikutano na mazungumzo ya kawaida. Benki imeendelea kutoa mafunzo, huduma za afya na mikopo kwa wafanyakazi wake. Katika kipindi hicho kulikuwa na utendaji wa pamoja kati ya wafanyakazi na menejimenti.

Benki imeendelea kutoa haki kwa kila mtu katika kupata ajira, kupandishwa vyeo bila upendeleo. Benki inahakikisha kuwa mtu yeyote mwenye sifa anapata au kupandishwa cheo bila kujali jinsia, hali ya ndoa, kabila, dini au ulemavu usiomfanya mtu asishindwe kufanya kazi.

### Mafunzo kwa wafanyakazi

Katika kipindi cha mwaka, Benki ilitumia TZS milioni 89.0 kwa mafunzo ya wafanyakazi (2021: TZS 70.3 milioni). Programu za mafunzo zimeandaliwa na zinaendelea kutengenezwa ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanapata mafunzo ya kutosha katika ngazi zote. Wafanyakazi walipata mafunzo ili kuboresha ujuzi na kuimarisha utendaji wao wa kila siku.

### Mikopo kwa wafanyakazi

Benki inatoa mikopo kwa wafanyakazi wake ili kujenga mazingiza bora ya kazi. Mikopo inayotolewa kwa wafanyakazi inazingatia taratibu

zilizopo na kwa muda maalum na hali halisi kama ilivyopitishwa na Bodi ya Wakurugenzi. Hadi sasa deni la mikopo la wafanyakazi ni TZS 1,098,055,316.47.

### Huduma za afya

Benki ina gharamia matibabu ya wafanyakazi wake wote na wategemezi wao wa karibu kupitia mfumo wa bima ya afya kwa wafanyakazi wote.

### Mafao ya kustaafu

Benki inachangia mafao stahili ya wafanyakazi wake kwenye mfuko wa NSSF. Wajibu wa Benki ni kumchangia kila mfanyakazi asilimia 10% ya mshahara ghafi kwenye Mfuko wa NSSF

## 5.19 USAWA WA KIJINSIA

Benki inatoa fursa sawa za ajira na kuhakikisha hakuna ubaguzi wa jinsia katika ajira. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2022 Benki ilikuwa na mgawanyo wa wafanyakazi kijinsia kama ifuatavyo: -.

| **Jinsia** | **2022** | **2021** |
|---|---:|---:|
| Wanawake | 71 | 70 |
| Wanaume | 96 | 94 |
| **Jumla** | **167** | **164** |

## 5.20 MISAADA YA KISIASA

Benki haikutoa mchango wowote kwa vyama vya siasa kwa mwaka 2022. Pia haikutoa mchango wowote kwa vyama vya siasa mwaka 2021.

## 5.21 UHUSIANO NA WADAU

Benki iliendelea kuwa na uhusiano mzuri na wadau mbalimbali wakiwemo wasimamizi wa shughuli za kibenki.

## 5.22 WAJIBU WA KIJAMII BENKI NA MICHANGO YA HISANI

Benki ilishiriki vizuri kwenye shughuli za kijamii na mipango ya maendeleo nchini. Katika kipindi cha mwaka 2022 Benki ilishiriki kuhudhuria na kutoa michango ya jumla ya shilingi millioni 23.42 ikilinganishwa na shilingi milioni 12.68 mwaka 2021. Benki ilitoa hisani kwa kutoa mchango ya kielimu kwa vituo mbalimbali vya mayatima.

## 5.23 UKAGUZI

PricewaterhouseCoopers alikuwa mkaguzi wa benki kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2022. Pendekezo la kumteua mkaguzi wa nje wa benki kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2022 liliidhinishwa na wana hisa kwenye mkutano wa 13 na iliamuliwa kuwa ndiye atakayekuwa mkaguzi kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2022.

Ripoti hii ya Bodi ya Wakurugenzi iliidhinishwa Mei 4, 2023 na kuwekwa sahihi kwa niaba ya bodi kutokana na azimio la Bodi ya Wakurugenzi na;

**Mr. Gasper Casmir Njuu**
**Mwenyekiti wa Bodi**

**Ms. Uphoo Swai**
**Mjumbe wa Bodi na Mwenyekiti wa BARC**

# TAMKO KUHUSU MAJUKUMU YA BODI YA WAKURUGENZI

Sheria ya Makampuni Na.12 ya 2002 inawataka Wakurugenzi kutayarisha taarifa za hesabu za kila mwaka zinazoelezea hali halisi ya Benki kifedha na usahihi wa faida au hasara. Sheria hiyo inawataka Wakurugenzi kuhakikisha kwamba Benki inaweka vema taarifa zake zote za kifedha kwa ajili ya kutoa taarifa sahihi na ya kuridhisha juu ya hali ya fedha ya Benki. Wakurugenzi pia wana wajibu wa kuhakikisha panakuwepo taratibu na kanuni za kulinda mali za Benki.Wakurugenzi wanakubali kuwa ni wajibu wao kutoa taarifa za hesabu za mwaka, ambazo zimeandaliwa kwa kuzingatia sera zilizokubalika za hesabu zinazohitaji maamuzi yenye busara katika makadirio kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa za aina hiyo (Internationa Financial Reporting Standards); na kwa mujibu wa Sheria za Makampuni ya mwaka 2002 na ile ya Benki na Taasisi za Kifedha ya mwaka 2006.

Ni maoni ya Wakurugenzi kuwa tarifa za fedha zinaelezea hali halisi ya kifedha ya Benki na faida iliyoipata kama zilivyotengenezwa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya uhasibu (IFRS).

Wakurugenzi pia wanakubali kuwa ni wajibu wao kuhakikisha kwamba uwekaji wa hesabu za uhasibu unakuwa sahihi na unaaminika kwa ajili ya maandalizi ya taarifa za hesabu na pia kuwapo kwa mifumo sahihi ya udhibiti wa ndani ili kuhakikisha uhifadhi wa mali za Benki.

Wakurugenzi wanathibitisha kwamba hakuna tukio lolote wanalolifahamu ambalo lingeweza kusababisha Benki kutoendelea kuwepo na kufanya shughuli zake katika kipindi cha miezi 12 ijayo kutoka tarehe ya taarifa hii.

**Mr. Gasper Casmir Njuu**
**Mwenyekiti wa Bodi**

**Ms. Uphoo Swai**
**Mjumbe wa Bodi na**
**Mwenyekiti wa BARC**

# TAMKO LA MKUU WA IDARA YA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2022

Kwa mujibu wa sheria ya Uhasibu na Ukaguzi namba 33 ya mwaka 1972 kama ilivyobadilishwa na sheria namba 2 ya mwaka 1995 inazitaka taarifa za fedha ziambatane na tamko la mkuu wa kitengo cha fedha aliyehusika kuziandaa taarifa hizo kwenye kampuni husika.Ni wajibu wa wahasibu kuisaidia Bodi ya Wakurugenzi kutekeleza wajibu wa maandalizi ya taarifa ya fedha ya kampuni inayoonyesha ukweli na uwazi wa ufanisi wa kifedha kuendana na kanuni za kimataifa za hesabu na sheria ya makampuni ya Tanzania ya mwaka 2002. Uwajibikaji wowote ule wa kisheria unaotokana na maandalizi ya taarifa hizi unabaki kuwa ni wa Bodi ya Wakurugenzi kama ilivyoanishwa hapo juu.

Mimi **Vitalis Constantine Michael** nikiwa Afisa mkuu wa fedha wa Benki ya biashara ya Mkombozi, natambua wajibu wangu wa kuhakikisha kwamba taarifa ya fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2022 imeandaliwa kuendana na kanuni za kimataifa za hesabu na sheria ya makampuni ya Tanzania ya mwaka 2002.Kwa hiyo ninathibitisha kwamba taarifaa hii ya fedha ni sahihi na inatoa uhalisia wa matokeo ya mtiririko wa fedha kwa Benki ya biashara Mkombozi kwa kipindi cha mwaka na tarehe iliyotajwa hapo juu na kwamba taarifa hii iliandaliwa kutokana na nyaraka halisi za fedha zilizopo Benki.

Imesainiwa na: ____________________

**Cheo: Ofisa Mkuu wa Fedha**

**Namba ya Uanachama wa NBAA: GA9176**

**Tarehe: Mei, 4 2023**

## AJENDA YA 6

# KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA TAARIFA YA FEDHA YA BENKI KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2022; NA KUPOKEA RIPOTI YA MKAGUZI WA NJE WA HESABU, JUU YA TAARIFA HIYO YA FEDHA.

### Maoni ya Mkaguzi

Tumekagua taarifa ya fedha ya Benki ya Biashara Mkombozi (Benki) kama inavyoonyeshwa kuanzia ukurasa wa **55 hadi 95** za taarifa hii. Tumekagua Taarifa ya Hali ya Kifedha ya Benki; Taarifa ya Mapato na Matumizi; Taarifa ya Mtiririko wa Fedha na Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji pamoja na Waraka wa Taarifa za Fedha na Muhtasari wa Mabadiliko ya Sera za Uhasibu kwa mwaka ulioshia Desemba, 2022.

Maoni yetu ni kuwa Taarifa za Fedha zinaonyesha hali halisi ya kifedha ya Benki kufikia tarehe 31 Desemba 2022. Taarifa za utendaji wa kifedha na ya Mtiririko wa Fedha zimetolewa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya kihasibu na kwa kulingana na matakwa ya Sheria ya Kampuni Na. 12 ya Mwaka 2002.

### Msingi wa Maoni ya Mkaguzi.

Tulifanya ukaguzi kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa vya kimataifa. Viwango hivyo vinatutaka sisi kufuata kanuni zinazotakiwa na kuandaa mpango wa kufanya ukaguzi ili kujiridhisha kama taarifa hizo za fedha hazina mawaa yanayoweza kuzuia ukweli wa ukaguzi.

Tunaamini kwamba matokeo ya ukaguzi tuliofanya ni timilifu na yanakidhi kutuwezesha kutoa maoni.

### Taarifa ya masuala ya kisheria na kanuni za kufuata

Taarifa hii pamoja na maoni imeandaliwa kwa ajili ya wanahisa wa Benki kwa mujibu wa sheria ya makampuni ya mwaka 2002; sheria ya Benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006. Kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni namba 12 ya mwaka 2002 tunatakiwa pia kutoa taarifa kama taarifa ya Wakurugenzi haiwiani na taarifa ya fedha.

- Tumechambua taarifa zote na maelezo ambayo kwa uelewa wetu wa kitaaluma ni muhimu kwa ukaguzi wetu;
- Kwa maoni yetu nyaraka zote za taarifa ya fedha za Benki zilihifadhiwa vizuri;
- Taarifa ya Wakurugenzi inaoana na taarifa ya fedha za Benki;
- Kwa mujibu wa sheria marupurupu ya Wakurugenzi yanapaswa kuonyeshwa kwenye taarifa ya fedha; na
- Taarifa ya fedha za Benki na mtiririko wa fedha unaoonyesha faida na hasara vinawiana na nyaraka za fedha.

Kwa maoni yetu mchanganuo wa mtaji wa Benki umenyambuliwa kulingana na Sheria ya uendeshaji wa Benki za Biashara ya mwaka 2006 na kanuni zitokanazo na sheria hiyo za mwaka 2014 na maelekezo mbalimbali yatokanayo na sheria ya Benki Kuu ya Tanzania. Mkaguzi mkuu ambaye alijikita katika kutoa taarifa hii ni Cletus Kiyuga.

Cletus Kiyuga ACPA- PP 1981

**Kwa niaba ya PricewaterhouseCoopers**

Wahasibu wa Umma aliyethibitishwa na Bodi ya Wahasibu

Dar es Salaam

**Tarehe: 5 Mei, 2023**

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI

| | Kipengele | 2022<br>TZS'000 | 2021<br>Imerudiwa*<br>TZS'000 |
|---|---|---|---|
| Mapato ya Riba kwa hesabu zinazozingatia faida halisi ya uwekezaji | 8 | 25,666,314 | 22,075,616 |
| Gharama za Riba kwa hesabu zinazozingatia faida halisi ya uwekezaji | 9 | (7,319,903) | (8,787,173) |
| **Mapato Halisi ya Riba** | | **18,346,411** | **13,288,443** |
| Hasara tarajiwa ya Mikopo – chechefu | 10 | (2,943,622) | (1,979,217) |
| **Mapato Halisi baada ya hasara tarajiwa ya mikopo** | | **15,402,789** | **11,309,226** |
| Marekebisho ya mali ya kifedha | | **1,020,898** | **(2,757,741)** |
| Ada na Tozo | 11 | 2,950,155 | 3,235,526 |
| Mapato mengine | 12 | 689,767 | 367,675 |
| Faida Halisi kutokana na Miamala ya Fedha za Kigeni | 13 | 1,033,281 | 800,258 |
| **Jumla ya Mapato Yasiyo ya Riba** | | **4,673,203** | **4,403,459** |
| **Faida Halisi ya Uendeshaji** | | **21,096,890** | **12,954,944** |
| Gharama za wafanyakazi | 14 | (7,877,382) | (8,407,309) |
| Punguzo litokanalo na kushuka thamani kwa mali zinazofanana na Fedha taslimu | 15 | (2,064,688) | (2,040,283) |
| Gharama nyingine za uendeshaji | 16 | (6,009,348) | (5,214,190) |
| **Jumla ya Gharama za Uendeshaji** | | **(15,951,418)** | **(15,661,782)** |

| | Kipengele | 2022<br>TZS'000 | 2021<br>Imerudiwa*<br>TZS'000 |
|---|---|---|---|
| **Faida/(Hasara) kabla ya Kodi ya Mapato** | | **5,145,472** | **(2,706,838)** |
| Tengo la Kodi ya Mapato | 17 | 476,421 | 847,328 |
| **Faida/(Hasara) kwa Mwaka** | | **5,621,893** | **(1,859,510)** |
| Mapato Mengine yaliyojumuishwa | | | |
| ***Vitu vinavyoweza kuanishwa upya kama sehemu ya faida au hasara*** | | | |
| -Thamani ya haki ya uwekezaji katika dhamana; | | | |
| -Thamani ya haki faida/(hasara) kwa mwaka | | 1,682,521 | (52,825) |
| -Kodi | | (504,756) | 15,847 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa baada ya kodi | | **1,177,765** | **(36,978)** |
| **Jumla ya Mapato/(Hasara) yaliyojumuishwa kwa mwaka baada ya Kodi** | | **6,799,658** | **(1,896,488)** |
| | | **TZS** | **TZS** |
| **Mapato yote ya jumla kwa Hisa** | **18** | **239** | **(79)** |

**Baadhi ya viwango hapa haviendani na taarifa za fedha za 2021 na zinaakisi marekebisho yaliyofanywa kusahihisha makosa katika miaka iliyopita, rejea kiambatanisho 40 kwa taarifa zaidi.*

## TAARIFA YA HALI YA KIFEDHA YA BENKI HADI 31, 2022.

| | Kipengele | 2022<br>TZS '000 | 2021<br>*Imerudiwa<br>TZS '000 | 01 Jan 2021<br>Imerudiwa*<br>TZS'000 |
|---|---|---|---|---|
| **MALI** | | | | |
| Fedha na salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 19 | 21,935,859 | 21,864,924 | 22,088,102 |
| Salio katika benki nyingine | 20 | 24,133,243 | 23,137,105 | 35,819,175 |
| Thamani ya hati ya uwekezaji katika Dhamana za Serikali | 23(a) | 12,099,332 | 9,970,853 | - |
| Dhamana za Serikali – Gharama zilizopunguzwa | 23(b) | 31,108,527 | 32,698,014 | 28,037,348 |
| Mikopo Halisi kwa Wateja | 22 | 115,038,724 | 106,859,941 | 118,743,143 |
| Uwekezaji katika dhamana za kampuni nyingine | 24 | 2,001,614 | 2,002,903 | 2,002,258 |
| Uwekezaji wa Hisa | 25 | 539,000 | 539,000 | 539,000 |
| Mali ya haki ya Kutumia | 26 | 4,290,588 | 4,164,289 | 4,382,734 |
| Mali Nyingine | 21 | 4,987,106 | 3,715,082 | 1,450,845 |
| Mitambo na Vifaa | 28 | 3,003,051 | 2,824,006 | 3,223,974 |
| Mali zisizoshikika | 27 | 440,639 | 818,153 | 900,351 |
| Kodi inayowezeza kurejeshwa | 17 | 1,017,432 | 647,743 | 641,682 |
| Mali ya Kodi iliyoahirishwa | 29 | 1,127,429 | 1,129,667 | - |
| **Jumla ya Mali** | | **221,722,544** | **210,371,680** | **217,828,612** |
| | | | | |
| **MTAJI NA MADENI** | | | | |
| **Madeni** | | | | |
| Amana za Wateja | 30 | 184,578,821 | 181,512,718 | 183,907,938 |
| Madeni | 31(a) | 1,497,942 | 3,833,014 | 8,894,206 |
| Mkopo mdogo | 31(b) | 2,913,750 | - | - |
| Dhima nyingine | 32 | 1,633,919 | 1,518,358 | 1,620,711 |
| Matengo | 33 | 788,285 | 751,470 | 536,220 |
| Dhima za Malipo ya Pango | 34 | 5,121,743 | 4,367,694 | 4,789,421 |
| | | **196,534,460** | **191,983,254** | **199,748,496** |

| Mtaji | Kipengele | 2022 | 2021 | 01 Jan 2021 |
|---|---|---|---|---|
| | | | *Imerudiwa | Imerudiwa* 2022 |
| | | TZS '000 | TZS '000 | TZS '000 |
| Mtaji wa Hisa | 35 | 23,555,002 | 23,555,002 | 20,615,272 |
| Punguzo la Hisa | 35 | (734,932) | (734,932) | - |
| Limbikizo la Hasara | | (1,498,956) | (9,055,650) | (6,066,474) |
| Akiba ya kiudhibiti | 36(a) | 2,726,183 | 4,660,984 | 3,531,318 |
| Akiba nyingine – FVOCI | 36(b) | 1,140,787 | (36,978) | - |
| | | **25,188,084** | **18,388,426** | **18,080,116** |
| **JUMLA YA DHIMA NA FEDHA ZA WANAHISA** | | **221,722,544** | **210,371,680** | **217,828,612** |

**Baadhi ya viwango hapa haviendani na taarifa za fedha za 2021 na 2020 na zinaakisi marekebisho yaliyofanywa kusahihisha makosa katika miaka iliyopita, rejea kiambatanisho 40 kwa taarifa zaidi.*

Taarifa hizi za fedha zimetolewa kwa idhini ya Bodi ya Wakurugenzi Mei 4 2023 na kusainiwa kwa niaba ya Bodi na:

**Bw. Gasper Njuu**

**Mwenyekiti wa Bodi**

**Bi. Uphoo Swai**

**Mjumbe wa Bodi na Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi**

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA ULIOISHIA DESEMBA 31, 2022.

| | Mtaji wa hisa TZS' 000 (Note 35) | Punguzo la hisa TZS' 000 (Note 35) | Mapato yaliyoshikiliwa TZS' 000 | Akiba ya kisheria** TZS' 000 (Note 36(a)) | Akiba ya thamani ya haki TZS' 000 (Note 36(b)) | Jumla TZS' 000 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio kuanzia Januari 1, 2021 - Kama ilivyotangazwa awali** | 20,615,272 | - | (3,573,857) | 3,531,318 | - | 20,572,733 |
| Mabadiliko ya mwaka uliopita (Kiambatanisho 40(III)) | - | - | (2,492,617) | - | - | (2,492,617) |
| Salio lililobadilishwa Januari 1, 2021* | - | - | (6,066,474) | - | - | 18,080,116 |
| Faida kwa mwaka: | | | | | | |
| Kama ilivyotangazwa awali | - | - | 3,046,104 | - | - | 3,046,104 |
| Mabadiliko ya mwaka uliopita (Kiambatanisho 40(I)) * | - | - | (4,905,614) | - | - | (4,905,614) |
| Kama ilivyobadilishwa* | - | - | (1,859,510) | - | - | (1,859,510) |
| Mapato mengine yanayostahili (yaliyobadilishwa)* | - | - | - | - | (36,978) | (36,978) |
| Jumla ya mapato mazima kwa mwaka (yaliyobadilishwa) | - | - | (1,859,510) | - | (36,978) | (1,896,488) |
| Mauzo ya hisa | 2,939,730 | (734,932) | - | - | - | 2,204,798 |
| Uhamisho kwenda kwenye akiba ya kisheria | - | - | (1,129,666) | 1,129,666 | - | - |
| **Salio hadi Desemba 31, 2021 (lililobadilishwa)** | **23,555,002** | **(734,932)** | **(9,055,650)** | **4,660,984** | **(36,978)** | **18,388,426** |

| | Mtaji wa hisa<br>TZS' 000<br>(Note 35) | Punguzo la hisa<br>TZS' 000<br>(Note 35) | Mapato yaliyo shikiliwa<br>TZS' 000 | Akiba ya kisheria**<br>TZS' 000<br>(Note 36(a) | Akiba ya thamani ya haki<br>TZS' 000<br>(Note 36(b) | Jumla<br>TZS' 000 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio hadi Desemba 31, 2021 - Kama il-ivyotangazwa awali** | 22,820,070 | - | (1,657,419) | 4,660,984 | - | 25,823,635 |
| Mabadiliko ya mwaka uliopita (Kiambatanisho 40(II)) * | 734,932 | (734,932) | (7,398,231) | - | (36,978) | (7,435,209) |
| Salio lililobadilishwa Januari 1, 2022 | 23,555,002 | (734,932) | (9,055,650) | 4,660,984 | (36,978) | 18,388,426 |
| Faida kwa mwaka | - | - | 5,621,893 | - | - | 5,621,893 |
| Mapato mengine yanayostahili | - | - | - | - | 1,177,765 | 1,177,765 |
| Jumla ya mapato yote kwa mwaka | - | - | 5,621,893 | - | 1,177,765 | 6,799,658 |
| *Uhamisho kutoka kwenye akiba ya kisheria | - | - | 1,934,801 | (1,934,801) | - | - |
| **Hadi Desemba 31, 2022** | **23,555,002** | **(734,932)** | **(1,498,956)** | **2,726,183** | **1,140,787** | **25,188,084** |

Akiba ya Hatari za Benki za Udhibiti inawakilisha kiasi kilichotengwa kwa ajili ya kufidia upotevu wa ziada wa hasara za mikopo ikiwa ni mwongozo wa Benki Kuu ya Tanzania. Akiba hipo kwenye mgawanyo.

*Baadhi ya viwango hapa haviendani na taarifa za fedha za 2021 na 2020 na zinaakisi marekebisho yaliyofanywa kusahihisha makosa katika miaka iliyopita, rejea koambatanisho 40 kwa maelezo zaidi.

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA MAPATO

| | Notes | 2022<br>TZS'000 | 2021 imerudiwa<br>TZS'000 |
|---|---|---|---|
| **Shughuli za Uendeshaji** | | | |
| Faida kabla ya kodi | | 5,145,472 | (2,706,838) |
| *Marekebisho:* | | | |
| Gharama ya riba kwenye deni za mikataba ya kukodisha | 9 | 426,557 | 597,227 |
| Matarajio ya hasara kwenye mikopo na mafao kwa wateja | 10 | 2,943,622 | 1,979,217 |
| Uchakavu katika mali yenye haki ya kuitumia | 14 | 885,268 | 776,713 |
| Uchakavu wa mali isiyoshikika | 14 | 377,514 | 387,114 |
| (Faida)/hasara isiyo ya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni | 34 | 17,488 | (26,222) |
| Uchakavu wa mali na mitambo | 14 | 801,906 | 876,456 |
| Riba iliyofutwa ya mikopo iliyotolewa kwa wateja | | 841,185 | 2,026,792 |
| Gharama ya riba katika mikopo | | 335,803 | 707,982 |
| Ongezeko la akiba | 33 | 511,815 | 384,000 |
| Mrejesho wa marekebisho ya mali ya kifedha* | | (511,269) | (86,954) |
| Mabadiliko (faida) hasara | | (1,020,898) | 2,757,741 |
| | | **10,754,463** | **7,673,228** |
| *Mabadiliko katika uendeshaji wa mali na madeni:* | | | |
| Ongezeko katika kiwango cha chini cha akiba kisheria | | (460,685) | (51,201) |
| Ongezeko katika mali nyingine | | (1,382,349) | (247,736) |
| Ongezeko/(pungufu) kwenye mikopo na mafao kwa wateja | | (10,942,693) | 5,206,405 |
| Ongezeko/(pungufu) kwenye amana kutoka kwa wateja | | 3,066,103 | (2,395,220) |
| Malipo ya kiinua mgongo | | (475,000) | (168,750) |
| Punguzo kwenye madeni mengine | | 115,560 | (102,354) |
| **Fedha kutoka kwenye shughuli za uendeshaji** | | **1,186,668** | **9,914,372** |

| | | 2022<br>TZS'000 | 2021<br>imerudiwa<br>TZS'000 |
|---|---|---|---|
| Kodi ya mapato iliyolipwa | 17 | (395,785) | (272,552) |
| **Mtiririko wa fedha taslimu kutokana na shughuli za uendeshaji** | | **790,883** | **9,641,820** |
| **Shughuli za uwekezaji** | | | |
| Punguzo/(Ongezeko) kwenye dhamana za serikali | | 1,143,528 | (14,684,344) |
| Punguzo/(Ongezeko) katika uwekezaji kwenye hati za kampuni | | 1,289 | (645) |
| Ununuzi wa mali isiyohamishika | 27 | - | (304,916) |
| Ununuzi wa mali na mitambo | 28 | (980,950) | (477,088) |
| **Mtiririko wa fedha taslimu kutoka (zilizotumika katika) shughuli za uwekezaji** | | **163,867** | **(15,466,993)** |
| **Shughuli za kifedha** | | | |
| Malipo ya madeni ya mikataba ya kukodisha - msingi | 34 | (431,413) | (955,773) |
| Malipo ya riba ya madeni ya mikataba ya kukodisha | 34 | (270,150) | (595,227) |
| Mapato kutokana na mkopo mpya | | 2,700,000 | - |
| Marejesho ya mkopo | | (2,457,124) | (5,769,174) |
| Utoaji wa hisa katika mwaka (Utoaji wa Hisa kwa wanahisa) | 35 | - | 2,204,798 |
| **Mtiririko wa fedha taslimu zilizotumika katika shughuli za kifedha** | | **(458,687)** | **(5,115,376)** |
| **Ongezeko la fedha taslimu na vinavyofanana na fedha taslimu** | | **496,063** | **(10,940,549)** |
| Ongezeko la fedha taslimu na vinavyofanana na fedha taslimu hadi Januari 1 | | 36,295,552 | 47,236,101 |
| Tofauti ya fedha taslimu za kigeni | | - | - |
| **Fedha taslimu na vinavyofanana na fedha taslimu Desemba 31** | **37** | **36,791,615** | **36,295,552** |

## TATHMINI JUU YA KUENDELEA KWA BIASHARA YA KIBENKI

Uongozi wa Benki na Bodi ya Wakurugenzi wamefanya tathimini ya Benki na kubaini kwamba inao uwezo wa kutimiza wajibu wake bila wasiwasi wa aina yeyote katika miaka michache ijayo. Taarifa hizi za fedha zimeandaliwa kwa mtazamo wa kutokuwapo kwa wasiwasi wa aina yoyote kuhusu uwezo wa Benki katika kutimiza wajibu wake.

Mtaji Mkuu wa Benki, Uwiano wa Mtaji Mkuu na Uwiano wa Jumla wa Mtaji ulikuwa TZS19,621 milioni (Uliorudiwa mwaka 2021 ni TZS12,190 milioni) ambao ni sawa na 13.05% na 14.84% (2021:9% na 9%). Mtaji wa Msingi kabisa ulikuwa ndani ya vigezo vya kiudhibiti vya TZS15,000 milioni. Vilevile, Uwiano wa Utoshelevu wa Mtaji navyo vilikuwa ndani ya vigezo vya kiudhibiti wa 12.5% na 14.5%.

Mtaji Mkuu na Jumla ya Mtaji vinategemea vigezo kadhaa pamoja na matokeo ya hesabu za fedha, kuongeza hisa za ziada na kiwango cha vihatarishi vinavyokubalika kubebwa na Benki. Wakurugenzi na Uongozi wa Benki wanatarajia kuboresha vigezo hivi kwa miaka michache ijayo.

Hali ya ukwasi wa Benki inatarajiwa kuendelea kuwa toshelevu kutimiza mahitaji na matakwa ya kibiashara. Hali inatarajiwa kuwa hivi kwa miaka michache ijayo. Wakurugenzi na Uongozi wataendelea kuchukua hatua stahiki za kupunguza athari hasi, ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa karibu wa vipimo vya Ukwasi, kupungua kwa Ukwasi, kufuatilia na kusimamia kwa karibu mtiririko wa shughuli za kila siku za Benki, kupunguza kasi/kutoa kipaumbele katika kukopesha ili kupunguza uwezekano wa baadhi ya wateja kushindwa kulipa madeni na upungufu wa ukwasi. Uongozi na Bodi ya Wakurugenzi watasimamia kwa ukaribu madeni ili kufanya marekebisho muhimu ndani ya muda mwafaka.

Cletus Kiyuga ACPA, PP1981

**Kwa niaba ya PricewaterhouseCoopers**

Wahasibu wa Umma aliyethibitishwa na Bodi ya Wahasibu

Dar es Salaam

**Tarehe: 5 Mei, 2023**

## 8. MAPATO YA RIBA

| | 2022 | 2021 |
|---|---|---|
| | | Imehakikiwa |
| | TZS'000 | TZS'000 |
| Mapato ya riba yanajumuisha: | | |
| Mikopo na madeni | 20,440,943 | 16,841,734 |
| Amana za Serikali na hati fungani za kampuni | 4,565,807 | 4,588,939 |
| Uwekezaji | 659,564 | 644,943 |
| | **25,666,314** | **22,075,616** |

## 9. GHARAMA ZA RIBA

| | 2022 | 2021 |
|---|---|---|
| | | Imehakikiwa |
| | TZS'000 | TZS'000 |
| Gharama za riba zilijumuisha: | | |
| Amana za muda maalumu | 5,974,997 | 6,508,072 |
| Amana za akiba | 575,747 | 600,654 |
| Amana katika benki nyingine | 6,800 | 375,238 |
| Kukopa | 122,052 | 707,982 |
| Mkopo mdogo | 213,750 | - |
| Riba ya limbikizo la mikataba ya ukodis-haji (Kiambatanisho 34) | 426,557 | 595,227 |
| | **7,319,903** | **8,787,173** |

## 10. HASARA YA MIKOPO INAYOTARAJIWA

| | 2022<br>TZS'000 | 2021<br>TZS'000 |
|---|---|---|
| Ongezeko la hasara linalotarajiwa kwa mikopo na madeni kwa wateja (Kiambatanisho 22) | 1,769,801 | 264,457 |
| Ongezeko la hasara linalotarajiwa kwa mikopo na madeni kwa benki (Kiambatanisho 22) | - | 3,614 |
| Kufuta mkopo ambayo haikuhakikishwa awali | 1,173,821 | 1,711,147 |
| | **2,943,622** | **1,979,217** |

## 11. MAPATO YA ADA NA TOZO

